



UKURASA 2



**WANAKIJIJI** wadai kuokota maiti kwenye maeneo yao kila wiki




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 22, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581198

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Hoja sita za rukhsa mikutano CHADEMA

## **MBOWE** aitaja CCM, polisi wampa ulinzi 'airport', hotelini hadi mkutanoni...*Endelea ukurasa 2*






Wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiwa kwenye mkutano wa hadhara Uwanja wa Furahisha jijini Mwanza jana uliohutubiwa na viongozi wa kitaifa wa chama hicho. **Picha kulia:** Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe (kulia) na Mwenyekiti wa Kanda ya Serengeti, John Heche wakiwasili uwanjani hapo. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Timu uchunguzi ulawiti shuleni yatinga mkoani

UKURASA 4

## Utata waibuliwa kuhusu mwalimu wa Hisabati anayedaiwa kujinyonga

UKURASA 3

**MICHEZO** NYOTA 9 NJE SIMBA IKIIVAA DODOMA JIJI UK. 24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Hoja 6 pazia mikutano CHADEMA

**Na Richard Makore,** MWANZA

BAADA ya serikali kutoa rukhsa ya mikutano ya kisiasa iliyokuwa imezuiwa kwa takriban miaka saba nchini, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimezindua rasmi mikutano yake, kikianza na hoja sita.

Katika uzinduzi huo uliofanyika jana kwenye Uwanja wa Furahisha jijini Mwanza, chama hicho kilitilia mkazo hoja hizo zinazojumuisha utoaji haki kwa wananchi, kasi ya ukuaji wa Deni la Taifa na uhaba wa ajira.

Pia yamo madai ya Katiba Mpya, Tume huru ya Uchaguzi na kupanda kwa gharama za maisha kutokana na mfumuko wa bei za bidhaa.

Akihutubia mkutano huo wa uzinduzi, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (pichani), alisema kila Mtanzania anapaswa kutendewa haki bila kujali itikadi yake ya kisiasa.

Mbowe alisema haamini katika kugawa watu na taifa katika vipande vipande kwa kuwa anaamini taifa ni moja na anataka liendelee kuwa moja.

Aliwataka wanachama na wafuasi wa CHADEMA kutowabagua wana CCM, hata kama huko nyuma waliwahi kuwafanyia madhila ya aina yoyote.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kuwapo maridhiano ya kisiasa, akidai kuwa wapo wana CCM ambao hawayataki kwa kuwa wanafaidika na kutokuwapo kwayo.

"Siwezi kumtukana Madam President (Rais), siwezi kufanya hivyo hata siku moja, kumshawishi Rais akakubali maridhiano halafu leo nimtukane!" Alisema Mbowe na kukumbusha kuwa alisimama kwa miaka 30 kutafuta haki na hakuna fedha wala mali itakayomfanya asaliti Watanzania.



Alisema amezaliwa familia yenye uwezo kiuchumi na alishawishiwa na watu wengi afanye usaliti, lakini hakufanya hivyo na 'hakuna asali ya kumbadilisha'.

Mbowe alisema alishangaa mtu aliyeitwa gaidi na kuwekwa mahabusu gerezani, lakini akaitwa Ikulu.

"Gaidi anaitwa Ikulu, nyie washikaji acheni masihara! Nikaheshimu mamlaka, nikaenda kumwona Madam President," alisema Mbowe akikumbusha kilichojiri kabla ya maridhiano hayo ya kisiasa.

Alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kupokea msafara wake kuanzia uwanja wa ndege bila bughudha yoyote, akisisitiza hiyo ndiyo nchi anayotamani kuiona.

"Hawa polisi wana risasi, wana mabomu, lakini leo (jana) hawajatugusa hata kidogo, tumeenda mpaka kule sijui wapi," Mbowe alisifu na kubainisha kuwa chama chake kitaendelea kupigania matatizo mengi ya nchi ikiwamo Deni la Taifa, uhaba wa ajira, kupanda kwa gharama za maisha na upatikanaji wa haki kwenye mahakama.

Akimkaribisha Mbowe, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alimwomba atangaze kila ifikapo Januari 21 kila mwaka iwe siku ya chama hicho kwa kuwa kilisajiliwa rasmi tarehe hiyo mwaka 1993, ukiwa ni mwaka tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi nchini.

Alisema vipaumbele vya chama hicho kwa sasa ni upatikanaji wa Katiba Mpya na Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Mnyika pia aliwataka wanachama na wapenzi wa chama hicho kujiandaa vyema kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani.

Msafara wa viongozi wa CHADEMA uliingia uwanjani Furahisha saa 2:52 alasiri na dakika sita baadaye ilipotimu saa 2:58 Mbowe aliwasili uwanjani.

Msafara wa viongozi wa chama hicho uliongozwa na gari la polisi lenye usajili namba PT 4312 huku jeshi hilo likiimarisha ulinzi uwanjani muda wote.

Mwenyekiti wa CHADEMA mkoani Mwanza, Grayson Warioba, alisema hawataki kuwa chawa kwa kuwa huyo ni mdudu mbaya na mchafu badala yake wanataka wawe nyuki ili washambulie.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi wa kitaifa wa chama hicho na waliokuwa wagombea wao wa ubunge nchi nzima mwaka 2020.

## Muswada marekebisho Sheria ya Huduma za Habari waiva

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari yatafanywa wakati wa mkutano ujao wa Bunge.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alibainisha hayo jana wakati wa mkutano wa wahitimu wa mafunzo ya uongozi na uzinduzi wa Women in News Alumni Tanzania uliofanyika Dar es Salaam.

Msigwa alisema mabadiliko yatakayofanywa yanalenga kuondoa vipengele ambavyo wadau katika sekta hiyo wamekuwa wakivilalamikia.

"Hii ni hatua kubwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameonyesha utayari wake kwenye ustawi wa vyombo vya habari nchini," alisema Msigwa.

Miongoni mwa yanayolalamikiwa katika sheria hiyo ni kuwapo vifungu vinavyowanyima waandishi wa habari uhuru wa kuchapisha taarifa mbalimbali.

Msigwa aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari nchini kuweka sera itakayohusu masuala ya jinsia ili kusaidia kukomesha vitendo vya unyanyasaji kwenye vyombo vya habari.

Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alisema mafunzo yanayotolewa na Women in News, yamemsaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yake ya kila siku hususani katika nafasi yake anayoiongoza kwa sasa.

"Mafunzo haya yameniongezea maarifa sana katika kazi zangu hususani katika kujiamini na kuweka vizuri mipango yangu ya kujiendeleza katika fani hii ya uandishi wa habari," alisema Beatrice.

Kuhusu unyanyasaji kwenye vyombo vya habari, Beatrice alishauri kuwapo vyombo maalum ndani ya vyombo hivyo ambavyo vitatumika kuchukua malalamiko kuhusu vitendo hivyo vya unyanyasaji.

Naibu Mtendaji Mkuu wa Women in News, Jane Godia, aliipongeza serikali kwa kusimamia uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake katika Vyombo vya Habari ambao pia ni wahitimu wa Women in News, Salome Kitomari, alisema lengo la kuzindua rasmi chama hicho ni kusaidia kuwainua waandishi wa habari ndani ya vyombo vya habari.

# Wananchi wadai kuokota maiti kila wiki

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MAUAJI mfululizo ya watu ambao maiti zao zinaokotwa kila wiki maeneo tofauti katika wilaya ya Manyoni mkoani Singida, yamewashtua wananchi wa wilaya hiyo ambao wamelazimika kupaza sauti kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba na kumwomba aingilie kati.

Katika hali ya kushangaza, wananchi hao wamesema mauaji ya watu yameibua hofu kubwa kwa jamii huku wakidai baadhi ya pikipiki zinazomilikiwa na askari polisi wilayani hapo kwa ajili ya kuendesha biashara zinatumika kwenye mauaji hayo.

Wananchi wa Manyoni walimweleza juzi hayo, Serukamba ambaye alifanya ziara wilayani humo kusikiliza kero mbalimbali ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake kwa wilaya zote kwa lengo la kusikiliza kero na kuzipatia ufumbuzi.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa hapa Manyoni vifo vimekithiri sana. Kila wiki lazima tuokote maiti mahali fulani lakini si kwamba wananchi wa Manyoni hawawafahamu wahalifu bali wanawafahamu," alisema Prisca Maleta.

Maleta ambaye wakati akizungumzia suala hilo, alikuwa akishangiliwa na wananchi wenzake, alisema wanashindwa kutoa taarifa polisi kutaja wanaohusika na uhalifu huo kwa sababu baadhi ya polisi si waaminifu, wanatoa siri za watoa taarifa.

"Tatizo linakuja kwa Jeshi la Polisi. Mimi Prisca ninapokwenda kutoa taarifa polisi kabla mtuhumiwa hajaenda kukamatwa, wanampa taarifa kuwa fulani amekuja kukuripoti. Vitendo hivi ndivyo vinasababisha vifo kuongezeka kwa sababu kunakuwa na visa na visa," alisema.

Maleta alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa kuna baadhi ya askari anawajua kwa sura na majina ambao wanamiliki pikipiki zao ambazo ndizo zinazohusika kwenye mauaji ya watu.

"Kuna baadhi ya askari kwa sura na majina ila siwezi kuwataja hapa. Ukihitaji nitakutajia wana pikipiki zao ambazo ndizo zinashiriki kwenye uhalifu," alisema.

Mwananchi mwingine, Khalfan Poloto, alilalamikia jeshi hilo kitengo cha upelelezi kuwa mtu anapopeleka taarifa kituoni na kufunguliwa jadala, badala ya kukutanishwa na askari mpelelezi wa kesi yake, hupewa namba ya simu na kila ikipigwa mhusika husema yuko nje ya wilaya.

Poloto alisema tatizo hilo limekuwa sugu kwenye idara ya upelelezi ya polisi wilayani hapa, hali inayowafanya waamini huduma haziwezi kuwa na ubora unaotakiwa kutokana na unyeti wa idara hiyo.

**OCD ANENA**

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Manyoni (OCD), Ahmad Makele, akijibu madai hayo, alikiri kuwapo kwa mauaji hayo.

"Vifo vinavyotokea si vya kisasi wala kuwania mali sababu mtu anauawa vinachukuliwa viungo vya mwili kama vile sehemu za siri," alisema.

Makere alisema Jeshi la Polisi limeanza kuchukua hatua za kukabiliana na mauaji hayo na kwa kadhaa wamekwishakamatwa na misako zaidi bado inaendelea kufanyika ili kukomesha vitendo hivyo.

**RC AAGIZA**

Kutokana na malalamiko hayo ya wananchi, Serukamba amemwagiza Ofisa Usalama wa Taifa wa Wilaya ya Manyoni (DSO), kuunda kamati itakayoshirikisha vyombo vyote vya usalama kuchunguza mauaji hayo.

Serukamba ambaye alionekana kuchukizwa na suala hilo, alisema mkoa anaouongoza hawezi kukubali kuwa na askari wanaoshirikiana na wahalifu.

"Haiwezekani watu wanauawa kirahisi rahisi na serikali ipo, vinginevyo tumwambie IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini) awaondoe Manyoni. Pia hatuwezi kuwazuia na polisi wanaoshirikiana na wahalifu, hatuwezi kuwafukuza kazi lakini tunaomba wapelekwe mikoa mingine.

Hapa tunahitaji kuona polisi wema ambao wanalinda wananchi na mali zao," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi lina uwezo wa kuwajua wahalifu, washirikina na wanaofukua makaburi, hivyo wote wafahamike na wachukuliwe hatua kali za kisheria.

## HABARI KITAIFA

# Aliyeshambuliwa na wafugaji adai kupewa RB ya ubakaji

**Na Halfani Chusi**

MKULIMA Hussein Mfaume anayedai kushambuliwa na kuvunjwa mkono na wafugaji wa jamii ya Wasukuma baada ya kulisha mifugo yao kwenye shamba lake lililoko Kijiji cha Minazi Mikinda, Kibaha mkoani Pwani, amedai kuwa baada ya kutoa taarifa Kituo cha Polisi Mlandizi, aliandikiwa RB ya ubakaji.

Tukio la kushambuliwa kwa mkulima huyo liliripotiwa na Nipashe Novemba 17, mwaka jana, baada ya kutokea Oktoba 23, mwaka jana.

Akizungumza kwenye ofisi za Nipashe zilizoko Mikocheni mkoani Dar es Salaam jana, Mfaume alidai kuwa baada ya kushambuliwa, alikwenda Kituo cha Polisi Mlandizi kutoa taarifa na kupewa RB namba 2058.

"Baada ya kupewa RB, niliambiwa kesi yangu itafanyiwa upelelezi, jambo lililonishangaza, baada ya siku chache mbele niliporudi kituo cha polisi, nilipewa RB nyingine namba 2258.

"Nilipofika kituoni na kumweleza mpelelezi kuhusu taarifa nilizotoa awali, alipoiangalia RB akagundua inahusu kesi ya ubakaji ndipo ikabidi atafute kwenye kumbukumbu zao na kunibadilishia taarifa," alidai.

Mfaume alisema kuwa licha ya kubadilishiwa taarifa, mpaka sasa ikiwa ni miezi mitatu, hakuna kilichofanyika hivyo ameliomba Jeshi la Polisi kumsaidia ili watuhumiwa wakamatwe na kuchukuliwa hatua.

Mkulima huyo pia aliwaomba wasamalia wema wamsaidie ili apate matibabu na kupitia namba yake ya simu 0758899997.

"Baada ya kushambuliwa, nilikwenda kituo cha afya kutibiwa, kutokana na kuvunjika, walinitaka niende Hospitali ya Tumbi kule Kibaha, lakini sikuweza kwenda mpaka sasa kwa sababu sina fedha.

"Nilikuwa fundi ujenzi, baada ya kufanya kazi, malipo yangu niliyatumia kununua shamba Minazi Mikinda mwezi Agosti mwaka jana na baadaye nikashambuliwa, wakati huo nikiwa nimetumia fedha karibu zote kulihudumia shamba," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alipotafutwa na Nipashe jana, alisema amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) kulishughulikia suala hilo.

"Nimeongea na OCD pamoja na huyu mkulima aliyeshambuliwa, taarifa nilizopewa ni kwamba jambo lake lilishughulikiwa kwa kiwango kikubwa na serikali ya mtaa.

"Kwa hiyo, nimemwambia arudi pale Kituo cha Polisi Mlandizi akamwone Mkuu wa Kituo ambaye tayari nimeshampa maelekezo na atoe ushirikiano wa kutosha mpaka watakapomkamata mtuhumiwa kwa sababu yeye ndiye anamjua kwa sura.

"Shida ninayoiona yuko peke yake, hana shahidi, kwa hiyo ushahidi wake utaungwa mkono na majibu ya daktari," alifafanua.

Kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji maeneo hayo, kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi limeshafika huko na kuwaamuru wafugaji waondoke kwa kuwa mbali na mifugo kuharibu mazao, huchangia kuharibika kwa miundombinu na vyanzo vya maji.



Katibu Mkuu Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Al Hajj Nuhu Jabir Mruma, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kwa niaba ya Mufti wa Tanzania Sheikh Abubakar Zubeir, kuhusu kuundwa kwa tume ya maboresho ya baraza hilo yenye wajumbe saba ili kuchunguza mikoa au wilaya zenye migogoro mikubwa ya uongozi au mali na kushauri namna bora ya kuitatua. Kulia ni Mkuu wa Itifaki wa baraza hilo, Muhamed Amran. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wafugaji yatumieni majosho ya serikali

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

SERIKALI imewataka wafugaji kupeleka mifugo yao kwenye majosho ya serikali yaliyojengwa maeneo mbalimbali ili kuikinga mifugo dhidi ya magonjwa yaliyotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jana na jamii ya wafugaji katika Kijiji cha Machenje wilayani Kongwa jijini Dodoma, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Chilo aliwataka wafugaji watunze mazingira ili kuruhusu majani kuota.

Katika ziara hiyo alishuhudia namna ng'ombe wanavyopita kwenye majosho na kupata fursa ya kukagua miradi mbalimbali ikiwamo uchimbaji wa visima kwenye maeneo ya vijiji vya Mtanana, Chigwingwili, Soiti, Ndalibo, Ugogoni, Machenje, Nguji, Ibwaga na Chitomolo.

Akizungumza na wananchi hao, Chilo aliwataka wale wanaomiliki mifugo ya miguu minne, wahakikishe wanaipeleka kwenye majosho hayo.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji waliofika kuogesha mifugo, Abdi Juma aliishukuru serikali kwa kuwaletea huduma hiyo ya majosho ambayo itaondoa hasara waliyokuwa wakiipata ikiwamo vifo vya mifugo.

"Tumekuwa tukipoteza mifugo kwa kufa kutokana na mazingira kuwa jangwa, kwa hiyo miradi hii ikiwamo ya sehemu ya kunywesha mifugo, majosho ya kuwakinga na magonjwa inasaidia kuondokana na tatizo hili," Juma alisema.

Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa jamii za wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kongwa ulizinduliwa mwaka 2021 na unatekelezwa kwa miaka mitatu hadi mwakani na takribani wafugaji na wakulima zaidi ya 45,000 wanatarajiwa kunufaika.

# Utata waibuka mwalimu wa Hisabati kujinyonga

**Na Beatrice Shayo**

MWALIMU wa Shule ya Msingi Tuwapende Watoto iliyoko Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Gephason Shita (29), amekutwa amefariki dunia chumbani kwake, akidaiwa kujinyonga huku kifo hicho kikizua utata kutokana na miguu kukutwa ikiwa imegota sakafuni.

Mwili huo ulikutwa Jumatano ya wiki hii nyumbani kwake Mtaa wa Kihonzile Zone ya Bwawani, Bunju B kwenye nyumba aliyokuwa amepanga.

Mwalimu Mkuu wa Shule aliyokuwa anafundisha, Emmaculate Mlete, aliliambia Nipashe jana kuwa Mwalimu Shita amekuwa naye shuleni huko kwa miaka minne na hakuwa na tabia za utoro, hivyo kutoonekana kwake kwa siku mbili kuliwatia hofu.

"Tulifungua shule Januari 9, mwaka huu, alikuwapo na alihudhuria vipindi vyake vyote na alifundisha hadi jioni, Januari 17 (Jumanne) hakufika kazini, nilipewa taarifa za kutokufika kwake na hata alipopigiwa simu iliita bila kupokewa na alipoandikiwa ujumbe mfupi haukujibiwa.

"Siku iliyofuata (Jumatano) baada ya kuona hajafika, nilimtuma mwalimu mwenzake nyumbani kwake na alipofika alikuta mlango umefungwa, ndipo alipompigia mchumba wa mwalimu huyo ili kujua kama walikuwa na mawasiliano.

"Alipomweleza kuhusu kutokufika shuleni kwa siku mbili na namna walivyomtafuta kwa njia ya simu bila majibu, mchumba wake naye akasema naye amekuwa akipiga simu ya Mwalimu Shita bila kupata majibu, hivyo akamwambia mwalimu wetu kuwa atampigia mdogo wake anayeishi Bagamoyo kujua kama alikuwa anafahamu alikokuwa," alidai.

Mwalimu Mkuu aliendelea kufafanua kuwa baada ya mdogo wake kupewa taarifa hiyo, alipokwenda usiku kwa kaka yake na kuchungulia dirishani, ndipo alipomwona ananing'inia mlangoni na ndipo walipowajulisha polisi.

"Walipomwona hakuwa ametokwa haja kubwa na hata ulimi haukuwa umejitokeza nje wala macho, mwili ulikuwa tayari umeanza kuharibika, tulipatiwa na tukaukabidhi kwa ndugu zake ambao tumeaga jana (juzi) na kusafirishwa kwenda Kigoma," alisema Mwalimu Mlete.

Alisema kuwa Mwalimu Shita alikuwa anafundisha darasa la saba na kutokana na ufundishaji wake, aliwafanya watoto wapende somo la Hisabati kama ilivyo kwa masomo mengine.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kihonzile, Hassan Mndondwa, alisema kuwa baada ya kupewa taarifa za tukio hilo, walipofika walikuta mwili ukiwa unaning'inia kwenye mlango wa chumba chake.

"Baada ya nyaya za dirisha kukatwa, chini kulionekana damu sakafuni na kwenye pazia, mwili wake ulikuwa unaning'inia, hajaloa damu kokote, pazia lake lilikuwa linagusa sakafu, watu wakahisi labda kuna kitendo kingine cha mauaji amekifanya na yeye kujitundika. Mguu mmoja ulikuwa unatokwa damu," alidai.

Mkazi wa Bunju B, Zafarani Madai alidai kuwapo utata katika kifo cha mwalimu huyo kutokana na kukutwa miguu imegusa sakafu ilhali akidaiwa kujinyonga.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alipotafutwa kwa njia ya simu kuzungumzia tukio hilo, simu yake iliita bila kupokewa.

MAKALA MAALUM

# Timu uchunguzi ulawiti shuleni yatinga mkoani

**Na Mary Mosha**, MOSHI

MWENYEKITI wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa kilimanjaro, Nurudin Babu, amesema amepokea timu ya wataalamu itakayosaidia uchunguzi kwenye shule mbalimbali zilizoko mkoani dhidi ya matukio ya ukatili wa kingono na udhalilishaji.

Januari 17, mwaka huu, serikali iliunda timu ya kuchunguza vitendo vya ukatili wa kingono na udhalilishaji wanaofanyiwa wanafunzi kwenye baadhi ya shule nchini.

Hatua hiyo ilikuja siku chache baada ya Nipashe kuchapisha ripoti maalum inayofichua vitendo hivyo dhidi ya wanafunzi kwenye baadhi ya shule za bweni na kutwa mkoani Kilimanjaro.

Mkoa huo una shule za awali 961 (za serikali zikiwa 869 na binafsi 92), shule za msingi 992 (za serikali 872 na binafsi 120) na shule za sekondari 352 (binafsi 127 na serikali 225) ambapo 71 ni zenye kidato cha tano na sita.

"Nimepokea timu ya wataalamu, wamefika hapa mkoani kwa lengo la kuchunguza vitendo vya ukatili wa kingono na udhalilishaji wanaofanyiwa wanafunzi kwenye baadhi ya shule mkoani hapo.

"Bado hatuwezi kusema watafanya kazi hiyo kwa muda gani, ila wapo na watakapokamilisha, watatupa taarifa na tutawajulisha," Babu alisema mjini hapa juzi na kuongeza:

"Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa maadili ya wanafunzi katika shule zetu yameporomoka, siwezi kusema kuna shule inafundisha au inafanya nini, ila lipo kwa ujumla wake, tunapata taarifa mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali kwamba kuna mambo yanafanyika huku.

"Lakini Jeshi letu la Polisi limeshakamata watu wengi wanaojihusisha na vitendo hivyo na kuna kesi nyingine zipo mahakamani."

Baada ya Nipashe kuchapisha ripoti maalum kuhusu kuwapo baadhi ya shule ambazo wanafunzi wamekuwa wakifundishwa kufanyiana 'uchafu' huo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliunda timu ya kuchunguza suala hilo ambayo ilianza kazi rasmi juzi ili kupata ukweli na ukubwa wa tatizo.

Babu alisema kuwa kufuatia taarifa za kuwapo kwa kadhia hiyo kuripotiwa na Nipashe, walipokea simu mbalimbali kutoka kwa raia zikitaja baadhi ya shule zenye nembo zinazohusishwa na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja zilizowekwa kwenye mbao za matangazo ya shule.

"Tulifuatilia na kupata maelezo ya kina juu ya nembo hizo kutoka kwa wamiliki wa shule na kuwapa masharti ya kuondoa mara moja na kuweka kwa namna ambavyo tunataka sisi ili kuondoa sintofahamu, wameshaondoa na kuweka kibao cheupe na maandishi meupe lakini tume pia itapita na kufanya uchunguzi zaidi," alisema.

**MWALIMU ANENA**

Fedelis Msaki (63), ni mwalimu mstaafu na mkazi wa Mailistita, anasema tatizo la udhalilishaji wa kingono haliishi kwenye shule binafsi na za bweni, bali hata za kutwa hasa zenye ufadhili pamoja na za serikali.

"Nimekuwa mwalimu kwa miaka mingi, nimefundisha shule hizi binafsi ila ipo haja ya serikali kuangalia na kujiridhisha juu ya ufadhili wa masomo unaotolewa na NGO pamoja na mwingiliano wa masomo (internship) unaofanyika kwenye shule hizo, wengi hufundishwa vitendo vya ukatili wa kingono na wakati mwingine huogopa kutoa taarifa kwa lengo la kukatishwa masomo yao kutokana na uduni wa familia zao.

"Wadhibiti ubora watazame kwa kina kuhusu uendeshaji wa shule na aina ya watoto wanaochukuliwa, vitengo vya siku kwa siku vinavyofanyika shuleni, vitabu vinavyotumika kujifunzia vingine vina mambo ya ovyo kwa ukuaji wa watoto wetu," anadai mwalimu huyo.

Anaendelea kudai kuwa baadhi ya shule zimejengewa maktaba na kuwekewa vitabu kwa ajili ya kujifunzia, lakini baadhi ya vitabu haviendani na mitaala ya nchini.

"Maktaba zinazojengwa huwekwa vitabu vingi visivyo na maadili na visivyoendana na maadili ya kitanzania, pia kuna hadithi zisizo na maadili.

"Pia wapo baadhi ya walimu wanaochukuliwa na kupewa mafunzo maalumu kwa ajili ya kuwasimamia wanafunzi kusoma vitabu hivyo pamoja na kutumia kompyuta zenye programu maalum, walimu hawa hulipwa vizuri na kupewa vikao vya mara kwa mara vyenye posho.

"Mimi nilikuwa mmoja wa walimu waliopewa mafunzo hayo, ninaongea kitu ninachokijua vyema. Tatizo hili ni gumu kulielewa kutokana na Watanzania wengi, hata walimu, hawana tabia za kusoma na kufuatilia kitabu kwa kitabu na wazazi wengi hawajui lugha zinazotumika huko, hivyo kumwacha mtoto kukua katika ulimwengu wa giza," anasema.

Mwalimu huyo anasema ikiwa serikali inataka kumaliza tatizo hili, inapaswa kuipitia mikataba ya mashirika yasiyo ya kiserikali yote yaliyoko nchini kwa kuangalia ni kwa namna gani wanafanya kazi na ni vitu gani wanavyokuja navyo nchini hasa kwa watoto.

Pia ana angalizo kwamba ni lazima serikali itazame upya upokeaji wa kompyuta na mitaala wanayofundishwa wanafunzi shuleni kuanzia ngazi ya awali ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kwa taifa baadaye.

"Unakuta shule ina wanafunzi 100, ina walimu 40, wanalipa bili za maji, watoto wanakula na maendeleo mengine ya shule, serikali iache kufumba macho, itazame jambo hili, wapo wengine wamejificha kwenye kivuli cha dini, makongamano na vitu mbalimbali lakini hutumika kwenye kueneza vitendo vya ovyo.

"Wakaguzi wapo kuanzia ngazi ya kata na wengine wanajua haya mambo ila wanafumba macho kwa rushwa na zawadi, tuache, tubadilike na tutunze kizazi cha kesho," Mwalimu Msaki anadai.



Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu

**SAUTI ZA WADAU**

Aisha Nureni, mfanyabiashara na mkazi wa KCMC, Manispaa ya Moshi, anasema watoto huhofia kutoa taarifa hizo za ukatili wanazofanyiwa, hivyo huzoea vitendo hivyo na kuwafanya wabadilike kitabia.

"Hivi vitendo vipo na vinafanyika sana, mtoto wa jirani yangu wa darasa la sita, tumebaini amepata shida hiyo akiwa shule moja hapa manispaa na kwa sasa amehamishiwa shule ya serikali. Wazazi waongeze umakini katika kuwalinda watoto," anadai.

Elimrina Masawe, mkazi wa Njiapanda wilayani Moshi, anasema suala hilo lipo kwa kiwango kikubwa ingawa watu wengi hawana uelewa wa utoaji wa taarifa, hivyo timu iliyoundwa na serikali isipokuwa makini, haitapata taarifa za kina.

"Ninafikiri kila shule watoto wapewe nafasi ya kuandika kwenye karatasi kuonyesha na kumtaja mtu aliyefanya vitendo hivyo au kutafuta utaratibu maalum wa kupima watoto wote hadi vyuo vikuu ili kuona ukubwa wa tatizo.

"Pia kuwekwe utaratibu wa kila baada ya miezi mitatu watoto kupimwa kama wanavyopimwa mimba shuleni, ifanyike hivyo hadi vyuo vikuu na vyuo vya kati. Ikibainika umefanya vitendo hivyo ni kosa la kufukuzwa shule au chuo," alishauri Elimrina.

Peter Lashayo ni mkazi wa Majengo kwa Mtei mjini hapa, anasema kuwa licha ya serikali kuchukua hatua hiyo, kuna hapa jamii ishiriki kuanzia ngazi ya kitongoji hadi taifa kuona namna ya kuweka ulinzi kwa watoto kwa kuhakikisha kunakuwa na utaratibu mzuri wa kutoa taarifa shuleni au nyumbani pindi kunapotokea matukio ya aina hiyo.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ya mwaka 2021/22, ukatili wa kingono ulikuwa tishio katika kipindi hicho na waathirika ni watoto.

Kituo hicho kiliripoti kuwa watu walio karibu na watoto ndiyo wafanyaji wakuu wa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi ya watoto. Watu hao ni pamoja na wanafamilia, wajomba, baba wa kambo, baba zao, madereva bodaboda na walimu wa kiume.

Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 10 ya walimu wa kiume ambao walidaiwa kufanya ukatili wa kingono dhidi ya watoto/wanafunzi wa kike na vitendo vya ukatili wa kingono, husasan ulawiti ambapo ilikusanya matukio 14 ya ulawiti wa watoto wa kiume, ambayo yaliripotiwa kwenye mikoa ya Tanga, Katavi, Mara, Manyara, Dodoma, Dar es Salaam, Morogoro na Njombe. Matukio manne kati ya hayo, yaliripotiwa mkoani Katavi.

**MSAIKOLOJIA ALONGA**

Lisbeth Mhando ni Mhadhiri wa Chuo cha Afya na Tiba Kilimanjaro na Msaikolojia Tiba, anasema utafiti unaonesha asilimia kubwa ya ukatili na udhalilishaji wa kingono hufanywa na watu wa karibu na mtoto, wakiwamo walimu, wasimamizi wa shule, wazazi au walezi.

Anasema dalili za kwanza za kuonyesha mtoto huyo anatendwa ukatili ni pamoja na kukosa kujiamini, kupoteza hamu ya chakula au kula sana, kuota ndoto mbaya mara kwa mara, kuogopa kukaa mwenyewe, kutolala gizani, ongezeko la hasira, kuwa mkorofi kupitiliza au ukimywa sana na kujitenga.

"Hizi ni baadhi ya dalili za mabadiliko ya kitabia ambazo zinapoonekana kwa mtoto, ni wakati muhimu wa kuchukua hatua stahiki za kuanza kumchunguza na kupata tiba ya kisaikolojia.

"Mtoto huyo asipopata msaada haraka, ukatili huo unaweza kuathiri ukuaji wake kihaiba. Wafanyaji wa vitendo hivi, huwatisha na kuwajengea hofu na kutoaminika hata kama wakitoa taarifa hizo.

"Pia, jamii imekuwa ikimtwika lawama anayefanyiwa badala kumpa nafasi ya kujieleza na kumchunguza tukio hilo, tukiwapa nafasi ya kujieleza, tunaweza kupiga hatua katika kuwasaidia watoto wetu," anashauri.

**WATOTO WAFUNGUKA**

Nipashe imezungumza na baadhi ya watoto wanaokiri kufanyiwa ukatili huo wakiwa shuleni, akiwamo mwenye umri wa miaka 16 anayedai kuwa wanafunzi wenzake walimfanyia ukatili huo akiwa mwanafunzi wa darasa la nne kwenye moja ya shule zilizoko jijini Tanga.

Mtoto mwingine mwenye umri wa miaka tisa (jina tunalihifadhi), anadai: "Nilikuwa ninasoma shule ya kulala (bweni), ikawa wale wakubwa wanatufanyia hivyo, nikaumia, niliporudi nyumbani nikamwambia mama akanichapa na akanihamisha shule, nikarudi ya kutwa ya serikali huku akinionywa nisiseme jambo hilo".

Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009, mbali na mambo mengine, inaelekeza haki ya mtoto kulindwa dhidi kudhalilishwa kijinsia na haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa. Sheria hiyo pia inaelekeza wajibu wa mzazi/mlezi wa kutunza mtoto.

HABARI KITAIFA

# Muliro: 2022 ulikuwa mwaka mgumu

**Na Maulid Mmbaga**

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amesema mwaka uliopita ulikuwa mgumu, wenye hekaheka, changamoto na majaribu mengi katika maeneo mbalimbali.

Amesema kuwa kutokana na ugumu huo, Jeshi la Polisi lililazimika kufanya kazi ya ziada kutimiza majukumu yake ya kisheria.

Akizungumza jana Kinondoni mkoani Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuwatunuku vyeti vya heshima maofisa wa Jeshi la Polisi 78 waliofanya vizuri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kijeshi, Kamanda Muliro alisema polisi walizingatia weledi na kanuni mbalimbali zilizowawesha kufika walipo.

Kamanda Muliro alisema silaha yao kubwa ya utendaji wa kazi ni kuzingatia sheria za kazi, huku akiwasisitiza maofisa wa Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na jeshi hilo.

Pia aliwasisitiza maofisa wa jeshi hilo kuongeza jitihada katika kusimamia mifumo ya kuzuia vitendo vya kihalifu, pamoja na kujisomea sheria mbalimbali zikiwamo za mwenendo wa makosa ya jinai, kanuni za adhabu, sheria za ushahidi na za vyama vya siasa ili ziwe silaha katika utendaji wa kazi zao.

"Niwasisitize maofisa wa Jeshi la Polisi tuzisome sheria hizo mbalimbali ili tutambue utendaji wetu wa kazi tuwe tunafanya kwa weledi na utulivu, lakipi pia kwa mafanikio zaidi. "Kama huna maarifa ya sheria hizo, watu watakushangaa au utajikuta unatoa kauli za ovyo ambazo zinajenga taswira mbaya kwa Jeshi la Polisi, silaha yetu kubwa ya utendaji wa kazi ni kuzingatia sheria za kazi," alisisitiza Kamanda Muliro. Aliwapongeza maofisa wa jeshi hilo kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kwa weledi, wakiwakilishwa na 78 waliopatiwa vyeti vya heshima.

Vilevile, alisema wajibu wao ni kuhakikisha raia wote nchini wanakuwa salama pamoja na mali zao na kwamba kazi kubwa inayofanyika ni kuzuia vitendo vya kihalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mtatirio Kintinkwi, alitaja vigezo vilivyotumika kuwapatia vyeti vya heshima maofisa 78, vikijumuisha nidhamu, uadilifu, weledi, uaminifu, uwezo na ushirikiano mzuri kwa wenzae.

Vingine ni uwezo wa kuhudumia wateja wa ndani na nje, umahiri, ujasiri wa kukabiliana na matukio makubwa ya uhalifu, umakini kwenye kazi, kufuata kikamilifu ratiba za kazi, uwezo wa kumudu majukumu hasa kwa muda wa ziada, usimamizi mzuri kwa walioko chini yao, waliolетea sifa Jeshi la Polisi na nchi pamoja na usafi.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, ACP Jumanne Muliro (kulia), akikadhi cheti cha heshima kwa Konstebo wa Polisi, Raphael Daudi, ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wake katika kujitoa kulitumikia jeshi hilo kwa weledi, katika hafla iliyofanyika Kinondoni, jana. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Wanakijiji walia na mwekezaji kuwatapeli

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MWEKEZAJI aliyetaka kujenga shule ya sekondari kwenye Kijiji cha Nduguti wilayani Mkalama mkoani Singida, anadaiwa kufanya utapeli baada ya ardhi aliyopewa na kijiji kufanya uwekezaji huo kuigeuza matumizi na kuanza kukodisha kwa watu kuendesha shughuli za kilimo kwa zaidi ya miaka 14 sasa.

Suala hilo liliibuliwa na Philipo Mkumbo (80), mkazi wa kijiji wakati wa kikao na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba anayeendelea na ziara yake ya kutembelea kila wilaya kusikiliza kero za wananchi akiwa ameambatana na wataalamu.

"Mkuu wa Mkoa kuna mwekezaji alikuja kwenye kijiji chetu, akasema anataka kujenga shule, akaomba ardhi, taratibu zikafanyika akapewa ekari 50. Cha kushangaza badala ya kujenga shule, eneo hilo anakodisha watu wanalima mashamba, wananchi tukihoji hatupewi majibu," alilalamika Mkumbo.

Mwanakijiji huyo alidai mwekezaji huyo, huku akimtaja kwa jina, alipewa ardhi hiyo na kijiji tangu mwaka 2009 na baada ya kukabidhiwa, wananchi walisubiri ajenge shule ya kisasa lakini wakashangaa anakodisha watu ambao wanalima hadi sasa.

Ofisa Ardhi Wilaya ya Mkalama, Imikigwe Mwanitu, alipotakiwa kutoa ufafanuzi kuhusu suala hilo, alikiri kufahamu kero hiyo na kwamba eneo hilo lilishapimwa.

Hata hivyo, ofisa huyo hakufafanua eneo hilo limepimwa kwa ajili ya kummilikisha mwekezaji huyo anayelalamikiwa na wananchi au kwa shughuli zinginezo.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, aliagiza ardhi hiyo irudishwe haraka kwa uongozi wa kijiji hicho kama sheria inavyoelekeza kuwa kama ardhi haijaendelezwa kwa muda mrefu, inapaswa kurejeshwa kwa walengwa.

Kero nyingine iliyoshtua kwenye kikao hicho, ni ya serikali ya Kijiji cha Iglansoni kudaiwa kupora familia ya Melisiana John mashamba zaidi ya ekari 60 na kisha kuanza kuyakodisha kwa wananchi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo huku fedha zinazopatikana zikinufaisha viongozi wa kijiji hicho.

Mkuu wa Mkoa alimwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mkalama, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na Ofisa Ardhi wa Wilaya hiyo kwenda kwenye kijiji hicho na kumrudishia mashamba mama huyo.

Serukamba pia aliwaagiza maofisa ardhi, watendaji wa vijiji na kata wilayani humo kuacha vitendo vinavyosababisha migogoro ya ardhi ambayo imetajwa kama chanzo cha umaskini kwa wananchi.

"Acheni vitendo vya uuzaji wa ardhi ambazo tayari zina umiliki wa watu wengine, mnapofanya haya mnakuwa ndiyo chanzo cha umaskini wa wananchi, watu wanataka kulima, kufanya maendeleo lakini mnawakwamisha mnaposhindwa kuwatatulia shida zao," alionya.

Serukamba aliwataka watumishi wilayani humo kutekeleza wajibu wao kikamilifu kwa kuwa kufanya hivyo, kutapunguza kero za wananchi.

# TEF yaelekeza macho bungeni

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, amesema macho na masikio ya wadau wa habari nchini, yanaelekezwa jijini Dodoma kusubiri Muswada wa Sheria ya Habari kusomwa kwa mara ya kwanza Januari hii.

Balile aliyasema hayo juzi kwenye Ofisi za TEF, Kisutu jijini Dar es Salaam.

"Mwezi huu tunatarajia kwamba Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itawasilisha Muswada wa Huduma za Habari bungeni kama Waziri alivyoahidi mara kadhaa.

"Mungu akipenda mwezi Februari utakuwa umepitishwa na kuwa sheria, basi tuanze huo utaratibu mwingine wa kuunda vyombo vinavyotakiwa ikiwamo Baraza Huru la Habari na utunzi wa kanuni zitakazokuwa zimetokana na mabadiliko mbalimbali," alisema.

Balile alisema ana imani kubwa na mchakato huo kwa kuwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan yanatekelezwa ipasavyo.

"Tunaona maelekezo ya Rais Samia yanatekelezwa, sasa na ni hamu yetu kuona kwamba muswada huo unaingia baada ya kushindikana Bunge la Februari mwaka jana, ukashindikana mwezi wa tisa na mwezi wa Novemba," alisema.

Akizungumzia mchakato huo, Balile alisema kuwa baada ya dhamira ya wazi ya Rais Samia katika kuhakikisha tasnia ya habari inakuwa huru, vikao viwili vinefanywa kati ya wadau wa habari na serikali.

"Vikao hivyo vilipitia mapendekezo ya wadau na kutetea mapendekezo hayo kisha serikali nayo ilitoa mapendekezo yake na mwisho tulifikia mwafaka.

"Ahadi iliyokuwapo tangu awali ni kupeleka mapendekezo hayo katika Bunge la Januari. Tunaamini Waziri Nape (Nnauye, Waziri wa Habari, Mwasiliano na Teknolojia ya Habari) bado ana msimamo uleule wa kiongozi wake mkuu (Rais Samia) katika kupeleka muswada huo bungeni," alisema Balile.

Pia alisema mwelekeo uliopo una matumaini makubwa ya kuwa na sheria ambayo itasaidia kuunda vyombo mbalimbali vinavyotakiwa katika mahitaji ya wanahabari likiwamo Baraza Huru la Habari pamoja na utunzi wa kanuni zitakazokuwa zimetokana na mabadiliko mbalimbali. Miongoni mwa marekebisho yaliyoshauriwa na wadau wa habari nchini ni marekebisho dhidi ya Kifungu cha 6(e) kinachoeleza magazeti kupatiwa leseni kila mwaka badala ya usajili wa moja kwa moja.

Pia marekebisho dhidi ya Kifungu cha 7(2)(b)(iv) kinachoelekeza vyombo vya habari kutangaza au kuchapisha habari na masuala yenye umuhimu kwa Taifa kadri itakavyoelekezwa na serikali, wadau wakieleza kuwa kipengele hiki kinaingilia uhuru wa uhariri.

Sheria nyingine zinazolalamikiwa ni pamoja na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Huduma za Posta (EPOCA, 2010), Sheria ya Makosa ya Mtandaoni (2015), Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa na Kanuni za Maudhui Mtandaoni (2018).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Polisi wameonyesha mfano ulinzi mkutano CHADEMA

**JANA** ni siku iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu na Watanzania hususan wapenzi wa demokrasia kutokana na kufunguliwa kwa pazia la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini, baada ya kuwa 'kifungoni' kwa takribani miaka saba.

Kisiasa ilikuwa kama siku ya kuzaliwa upya kwa demokrasia hasa kwa uhuru wa kukusanyika na wa kujieleza ambao serikali ya awamu ya tano ilitangaza kuuweka kando kwa kile kilichodaiwa kuwa ni kuchelewesha maendeleo ya kiuchumi ikizingatiwa kuwa muda wa kufanya siasa ulikuwa umemalizika baada ya uchaguzi mkuu, hivyo vyama vinatakiwa kusubiri tena wakati wa kampeni.

Mkutano hiyo iliruhusiwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan baada ya aliyekuwa mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli kuweka zuio kwamba baada ya uchaguzi kumalizika kinachofuata ni kujielekeza katika masuala ya maendeleo ya wananchi.

Kutokana na zuio hilo, hakuna mikutano ya ndani wala ya hadhara ya vyama vya siasa iliyofanyika. Wakati mwingine, Jeshi la Polisi lilikuwa likizuia kufanyika hata kwa mikutano ya ndani kwa kile kilichodaiwa kuwa kuwapo kwa taarifa za kiintelijensia za uvunjifu wa amani.

Licha ya madai hayo, hivi karibuni wakati baadhi ya viongozi wa chama hicho wakiwa katika mikoa ya kusini, ilishuhudiwa mkuu wa polisi wa wilaya moja akizozana na kiongozi mmoja wa CHADEMA. Alichokuwa akikazania ni kusema hakuna kibali cha kufanya kikao cha ndani bila kueleza sababu za kuzuia kufanyika kwa kikao hicho.

Pazia hilo la mikutano ya vyama vya siasa lilianza rasmi jana kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo kuzindua mkutano wake wa hadhara kitaifa, uliofanyika katika viwanja vya Furahisha, jijini Mwanza, mkutano huo ulihutubiwa na Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe, huku ukihudhuriwa na viongozi wa ngazi za juu kitaifa na kikanda pamoja na wanachama, wapenzi na wafuasi.

Kwa jumla, ilikuwa furaha na bashasha kwa wanachama wa chama hicho kutokana na hasa mambo makuu mawili. La kwanza, ni kuwapo kwa nuru ya kidemokrasia na uhondo wa mikutano ya namna hiyo walioukosa kwa miaka saba lakini la pili ni mara ya kwanza kwa kiongozi huyo mkuu wa kitaifa wa chama kuwa jukwaani tangu alipoachiwa huru kutokana na kesi ya ugaidi iliyokuwa ikimkabili.


Wakati akitangaza kuondoa zuio la mikutano hiyo, Rais Samia aliagiza kila taasisi inayohusika, likiwamo Jeshi la Polisi, itimize wajibu wake na kusiwapo kikwazo kitakachoinuka na kutia doa nia hiyo ya kufufua na kuendeleza demokrasia nchini.

Katika mkutano wa jana wa CHADEMA, polisi walionekana kufanya kazi yao kikamilifu kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama inaimarishwa. Tangu wakati Mbowe anawasili Uwanja wa Ndege wa Mwanza hali ya ulinzi iliimarishwa na hata msafara wake uliongozwa na gari la polisi mpaka anafika hotelini. Pia kwenye uwanja wa mkutano, polisi walionekana kulinda amani kwa kuwaweka wafuasi sawa kwa kuhakikisha usalama unatamalaki.

Hakika, kwa polisi huo ni mwanzo mzuri katika kutekeleza wajibu wao na wameonyesha mfano wa nini kinatakiwa kufanyika ili kuimarisha usalama katika mikusanyiko badala ya mazoea yaliyokuwapo wakionekana wakipambana na wafuasi wa vyama vya siasa huku wakitembeza virungu na kuwasweka ndani baadhi ya wanachama hao.

Kwa kufanya hivyo jana, polisi wanastahili pongezi. Jambo la msingi, jeshi hilo lililopewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao, liendelee na mfano waliouonyesha jana kwa kulinda amani na kuacha kutumia nguvu kupita kiasi ambazo wakati mwingine husababisha maafa hata kwa wasio na hatia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Machinga wasaidiwe kuachana na mtindo huu

**IMEKUWA** kama jambo la kawaida kwa wafanyabiashara wadogo kung'ang'ania katika maeneo yasiyo rasmi, huku wakibuni mbinu mbalimbali za kuwafanya waendelee kuwapo maeneo hayo.

Mfano mmojawapo ni Dar es Salaam. Baadhi yao badala ya kwenda kwenye masoko waliyotengewa, wanaamua kuwa 'mafichoni' wakati wa asubuhi na kisha jioni kuanzia saa 11:00 jioni huibuka na kurejea katika maeneo ya awali.

Machinga hao ni mchanganyiko wakiwamo wale ambao wana meza za biashara kwenye masoko mapya na wengine wanaodai kuwa hawana meza hizo, wote kwa pamoja wamekuwa wakitumia mbinu hiyo. Kimsingi, mbinu hizo wanazotumia zinaweza kuwakwamisha kwa kukosa sehemu ya kuuzia bidhaa zao na kubaki wakiwa watu wa kutangatanga huku na kule, iwapo serikali itaamua kukomaaa nao.

Baadhi yao wanakiri kuwa na meza za biashara, katika masoko mpya na huweka vitu vichache, ili waonekane wapo na kisha wanaondoka na kwenda kujibanza vichochoroni wakisubiri jioni ifike warudi katika maeneo ya awali.

Wenye mbinu hiyo ni machinga wanaofanya biashara Mbezi Mwisho, ambao ninadhani ipo haja ya kuelimisha ili waondokane na mtindo huo na kwenda kwenye masoko yao na kuwafanya wateja wao wazoee mazingira hayo.

Muda wanaoutumia wakiwa mafichoni ni mwingi na unapotea bure, kutokana na ukweli kwamba, wanaporudi katika maeneo ya awali, wanafanya biashara kwa saa chache giza linaingia.

Ingekuwa vyema kama wangetambua hilo kuwa mbinu hiyo inaweza kuwakosesha wateja, kwani inaweza isiwe na faida na badala yake wakajikuta wakipata hasara zaidi ya kuharibikiwa na bidhaa.

> **Ingekuwa vyema kama wangetambua hilo kuwa mbinu hiyo inaweza kuwakosesha wateja, kwani inaweza isiwe na faida na badala yake wakajikuta wakipata hasara zaidi ya kuharibikiwa na bidhaa.**

Katika jambo hilo, ni muhimu pia wao kusoma ishara za nyakati, kwani zama zimebadilika, uwezekano wa kurejea kinyemelea kwenye maeneo ya awali umekuwa ni mdogo kwani kila mara wamekuwa wakivamiwa na kuondolewa

Ikumbukwe kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Slaam, Amos Makalla ameshatangaza kuwa kila Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi ni siku maalumu ya kufanya usafi kwa wakazi wa mkoa huo.

Machinga wamekuwa wakituhumiwa kufanya uchafuzi wa mazingira. Hivyo kwa hali kama hiyo, ingependeza kama watahama na kwenda kufanya biashara kwenye masoko waliotengewa.

Hatua hiyo itawasaidia pia kuachana na mtindo wa kufanya biashara kwa kuvizia, kwani suluhu ni kwenda kwenye masoko huku wakiendelea kuidai serikali kuyafanyia maboresho masoko hayo.

Ni kweli masoko ni machache, hayana miundombinu ya kutosha, lakini si vibaya wakayatumia, huku wakiendelea kudai yaboreshwe, kwa kuzingatia kwamba haki huwa inakwenda sambamba na wajibu.

Ninaamini kuwa kudai haki bila kutimiza wajibu si vyema, vinginevyo ni sawa na kusababisha malumbano yasiyo ya tija kati ya aliyeshika mpini na aliyeshika makali, na itakuwa rahisi kwa aliyeshika makali kuumia.

Machinga wanatajwa kama watu muhimu na ni suluhisho la mahitaji kwa watu wengi kuanzia wenye kipato cha chini, kati na kipato cha juu na wana umuhimu katika kukuza pato la taifa.

Ninaamini kwamba, badala ya kuendelea kufukuzana na serikali, wakitulia sehemu moja wanaweza kukuza uchumi wao na hata wa taifa na kusaidia kuondoa umaskini.

SAFU

KWA MASLAHI YA TAIFA

# Mambo haya yalipitaje mbele ya wanasheria nguli, wabobezi?



Pascal Mayalla

LEO naendelea na sehemu ya pili ya mada ya wiki iliyopita kuhusu haki kuu mbili za kisiasa zilizotolewa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na jinsi haki hizo zilivyotolewa na kifungu kimoja na serikali ya wakati huo, ikaja kuzipora kwa kuzitungia sheria batili. Baada ya ubatili huo kubatilishwa na Mahakama Kuu ya Tanzania, serikali hiyo ikapeleka muswada bungeni kwa hati ya dharura na kuliomba Bunge kufanya mabadiliko ya katiba ambayo nayo ni batili, kisha ubatili huo ukachomekewa kiubatili ndani ya katiba yetu ili kuihalalisha batili hiyo.

Haya yote yalifanyika huku Tanzania ikiwa nchi ya kwanza kwa Afrika Mashariki kufundisha somo la sheria. Kwa maana hiyo, tuna manguli wa sheria wabobezi na wabobevu. Pamoja na kuwa na wanasheria nguli, wabobevu na wabobezi, haya mambo ya ajabu yaliwezekana vipi kufanyika?

Kwa mujibu wa ibara ya 64.-(1) Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania, yatakuwa mikononi mwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ila ibara ya 64.- (5) inasema Katiba hii itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba hii, Katiba ndiyo itakuwa na nguvu, na sheria hiyo nyingine, kwa kiasi inachokiuka Katiba itakuwa batili.

Tafsiri ya ibara hii kwa mtu wa kawaida ni Katiba ndiyo sheria mama. Ikitokea sheria nyingine yoyote iliyotungwa, ikakinzana na Katiba, sheria hiyo nyingine inakuwa batili moja kwa moja. Kisheria wanaita 'null and void ab initio', yaani sheria hiyo batili inakuwa kama haipo na haijawahi kuwapo!

Ibara ya 5 ya Katiba imetoa haki kuu kwa kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 kuwa anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofaywa Tanzania na wananchi. Haki hii ya kuchagua, inakwenda sambamba na haki ya kuchaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 21.-(1) kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao.

Haki hizi mbili zilizotolewa na Katiba, japo haki ya kuchagua bado ipo, haki ya kuchaguliwa imeporwa kwa kuwekwa shurti batili kwenye ibara ya 39 na 67 kwa kuwekewa shurti la kudhaminiwa na chama cha siasa. Wakati wote wa kuwekwa kwa ubatili huu ndani ya katiba yetu, Tanzania tulikuwa na wanasheria tena manguli, wabobezi na wabobevu, kuanzia serikalini, bungeni na mahakamani.

Katika hilo, kulifanyika mambo makubwa sita. Kwanza, umetungwa muswada wa sheria inayokwenda kinyume cha Katiba. Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985. Mchakato wa utungaji wa sheria inawahusisha wanasheria na unaanzia serikalini. Sasa ilikuweje wanasheria wetu wakatunga sheria inayokinzana na katiba?

Pili, muswada huo wa sheria ukatua bungeni, kwenye wanasheria nguli, wabobezi na wabobevu. Bunge letu tukufu likatunga sheria hiyo batili ya uchaguzi. Mchakato wa utungaji sheria wa Bunge pia unahusisha wanasheria kwa kila hatua chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kila sheria inayotungwa na Bunge letu lazima iendane na katiba. Sasa sheria hii iliwezekaje kutungwa ili hali Bunge letu limesheheni wanasheria manguli wabobezi na wabobevu?

Tatu, mwanasiasa machachari, Mchungaji Christoper Mtikila (Mungu amrehemu) mwaka 1993, alifungua kesi Na. 5 ya 1993, kupinga kipengele kinachomtaka mgombea uchaguzi kudhaminiwa na chama cha siasa. Mahakama Kuu kupitia kwa Jaji Kahwa Lugakingira (Mungu amuweke mahala pema peponi), ikatamka wazi na bayana kipengele hicho ni batili na kinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, hivyo kifutwe na kutoa haki kuwa kila Mtanzania ana haki ya kushiriki kugombea uongozi.

Nne, Mahakama Kuu inapotamka sheria fulani ni batili kwa kwenda kinyume cha Katiba, kipengele hicho kilipaswa kufutwa pale pale kwa mujibu wa ibara ya 64.- (5) katiba itekelezwe pale pale kwa sheria hiyo kuwa batili kuanzia ilipotangazwa. Mara baada ya uamuzi huo wa Mahakama Kuu kuutangaza ubatili huo, ndipo sarakasi za mambo ya ajabu ya kisheria zilianza. Mtu anapokutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo jela, hupelekwa jela, kuanza kutumikia kifungo hata kama atakata rufani, hivyo uamuzi huu wa mahakama ulipaswa kuanza kutekelezwa pale pale!

Tano, Mahakama Kuu chini ya Jaji Lukakingira, ilitamka kuwa sheria hiyo ni batili kwa sababu inakwenda kinyume cha katiba. Mamlaka pekee nchini Tanzania yenye mamlaka ya kutafsiri sheria na kueleza ubatili wa sheria yoyote ambayo inakwenda kinyume cha katiba, ni Mahakama Kuu ya Tanzania, baada ya hukumu ya Jaji Lugakingira, kama katibu ndiyo sheria mama, ni wanasheria wa aina gani walioishauri serikali kukata rufani?

Sita, hili ni tundu kwenye paa letu la mhimili wa Mahakama, baada ya mahakama kuutangaza ubatili huo, kitu kikisha kuwa batili, ni kama hakipo na hakijawahi kuwapo, hatua ya kwanza ni kwanza hiyo sheria kubadilishwa kwa kuwa 'null and void ab initio', hivyo ilibidi ifutwe pale pale.

Hapa sasa serikali ilianzisha sarakasi! Je, serikali yetu ilianzisha sarakasi gani kwenye hili? Tukutane wiki ijayo kwa sehemu ya tatu na ya mwisho ya haki kuu ya kikatiba ya Watanzania. Tunataka jicho la haki la Rais Mama Samia, liliangazie hili.

**Wasalaam**

**Paskali +255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Marekebisho ya sheria sawa, tugeukie maadili, weledi



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MWEZI ujao, wanahabari nchini watakuwa na jambo lao bungeni Dodoma. Ni mwezi ambao Bunge la Jamhuri ya Muungano litakuwa na mkutano wake wa 10 unaotarajiwa kuanza Januari 31. Kwa maana hiyo zimebaki siku chache tu kabla ya kuanza mkutano huo.

Wanahabari watakuwa na jambo lao kwani ndipo serikali itakuwa inawasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Habari ya Mwaka 2016 ambayo imekuwa ikipigiwa kelele kuwa inabana uhuru wa habari.

Tayari serikali kupitia kwa Waziri mwenye dhamana ya habari, Nape Nnauye - Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imewahakikishia wanahabari kuwa muswada huo utakuwa mezani mwezi ujao. Sheria hiyo namba 12 itakuwa inaangaliwa na wabunge kwa lengo la kuirekebisha.

Lakini ikumbukwe kuwa hatua hiyo inafikiwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kukubaliana na maombi ya wanahabari na wadau wa habari nchini ya kuangaliwa upya kwa sheria hiyo ili wanahabari wafanye kazi zao kwa uhuru lakini wakizingatia maadili ya kitaaluma.

Mambo makuu yanayotazamiwa kuibuka katika muswada huo, baada ya majadiliano ya muda mrefu baina ya wanahabari na wadau upande mmoja na serikali upande mwingine, ni pamoja na la Mkurugenzi wa Idara ya Habari-MAELEZO kusajili na kufunga chombo cha habari.

Hapo itatakiwa kiundwe chombo huru cha kusimamia vyombo vya habari kitakachohusika pia na kusuluhisha pande zinazokinzana baina ya chombo na mlalamikaji anayedai kutendewa visivyo na chombo husika.

Suala la leseni kwa vyombo vya habari kama inavyotajwa na kifungu cha sita cha sheria hiyo, nalo litaibuka likitaka chombo cha habari kupewa usajili wa kudumu, badala ya leseni ya kila mwaka ili kuondokana na tabia ya kufunga vyombo lakini itasaidia kuvutia uwekezaji.

Pamoja na hayo, liko suala la uhuru wa mtu kufanya mawasiliano bila kuingiliwa, kinyume na Ibara ya 18(c) ya Katiba ya nchi. Lakini kuna kifungu kinachotaka uwekezaji wa mzawa na mgeni kuwa na uwiano wa asilimia 49 kwa 51, mzawa akitakiwa kumiliki 51.

Haya ni baadhi ya mambo muhimu yatakayojitokeza katika Muswada huo, utakaowafanya wabunge kubungua bongo zao na kuona ni lipi jema katika kuimarisha sekta ya habari nchini na kupanua wigo wa uhuru wa kujieleza, kupata na kutoa taarifa.

Bila shaka ni matumaini ya wanahabari kuwa serikali iliyoko kwa mwelekeo inaoounyesha katika ujenzi wa demokrasia na uhuru wa kujieleza, wabunge wataupitia muswada na kuutendea haki kwa mustakabali mwema wa tasnia na taifa kwa jumla.

Kupita kwa muswada huo na kuzaliwa sheria mpya itakayozingatia mwelekeo wa Tanzania mpya kitasnia, si tu itakuwa faraja kwa wanahabari bali pia kwa Watanzania wote wanaoamini katika utawala bora lakini pia wanaoomba Tanzania kuwa na mustakabali mwema.

Pamoja na faraja hiyo, wanahabari nao watatakiwa kuacha kulewa na kudhani sasa watakuwa juu ya sheria na kujiamulia chochote wakitakacho, ili mradi wanalindwa na sheria inayowapa uhuru, la hasha, mipaka itakuwapo.

Bado kanuni za kulinda maadili ya taaluma ya habari zitaendelea kuwapo, kwamba hakuna atakayeruhusiwa kuandika au kutangaza uongo, uzushi au hata kumchafua mtu, taasisi au chombo kingine kwa kuwa tu kuna uhuru.

Maadili ya kitaaluma ni muhimu katika kuhakikisha linajengwa Taifa lenye amani na utulivu, hivyo mizania ya habari itaendelea kuheshimiwa, ukweli utahitajika lakini pia weledi, kauli na mwonekano wa wanahabari vitaendelea kutamalaki.

Kupitishwa kwa muswada huo kuwa sheria, bila shaka kutakuja na chombo huru cha kusimamia maadili hayo, hivyo hatutatarajia tena kuona au kusikia waandishi au wanahabari wakibananga lugha wala kupotosha habari zao kwa maslahi binafsi.

Hatutarajii kuona au kushuhudia mwanahabari akijiita mwanahabari mwenye mwonekano wa kihuni kiwajihi na hata kimavazi, kwani kufanya hivyo ni kuitweza taaluma na kuivunjia heshima kwa jamii.

Bila shaka pia, hatutarajii kusikia vipindi vya redio au televisheni vikiendeshwa kama vijiwe vya wahuni na walevi, kwa kubishana na kupigizana kelele bila mpangilio wala weledi, kwa kuwa tu kuna fursa ya kuwa mbele ya vipaza sauti.

Ni matumaini ya kila mmoja kuona kuwa blogu na tovuti zinaacha kuandika uzushi, matusi, kejeli na kila mambo yanayokosa staha kwa hadhira, kwani kufanya hivyo kutakuwa ni kuua juhudi za muda mrefu zilizofanywa na wanahabari, wadau wa habari na serikali mpaka kufikia hapo.

**Alamsiki!**

# Jaji Kiongozi aonya watumishi mahakama kuendekeza rushwa

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JAJI kiongozi Mahakama Kuu Tanzania, Mustepher Siyani, amewataka watumishi wa mahakama nchini kutowaangusha Watanzania kwa kuendekeza ubinafsi, rushwa na upendeleo na kuwafanya wananchi kutokuwa na imani na utendaji wa mahakama.

Siyani aliyasema hayo juzi katika uzinduzi wa jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi, Lindi na Songwe uliofanyika Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi.

Alisema kwa uzuri na mwonekano wa majengo hayo uwe kielelezo cha kutoa huduma bora kwa wananchi huku akiwakumbusha wanapotumia majengo hayo wakumbuke kuwa yanatokana na kodi za wananchi watakaokuja mbele yao kutafuta haki.

"Kuna kazi ambazo kila mmoja anaweza kuzifanya lakini uhakimu sio moja ya kazi hizo. Kwa hiyo ni lazima sana kujipima na kutafakari katika zama hizi tulizonazo, mtumishi wa mahakama anapokamatwa au kutuhumiwa kwa rushwa anachafua na kurudisha nyuma imani ya wananchi wanayopaswa kuwa nayo," alisema Jaji kiongozi.

Alisema hadi kufikia Septemba 2022 mahakama ilikuwa imefikisha huduma kwa mahakama za hakimu mkazi kwenye mikoa 26 na mahakama katika wilaya 134 kati ya wilaya 139 zilizoko nchini.

Alisema ujenzi wa mahakama za hakimu mkazi katika mikoa mitatu ya Katavi, Lindi na Songwe utasaidia kupunguza umbali wa huduma na zaidi ni kuharakisha kazi ya usikilizaji wa mashauri.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa mahakama ya hakimu mkazi Katavi, wananchi zaidi ya 700,000 walilazimika kufuata huduma hiyo kwenye Mkoa wa Rukwa.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha inaimarisha miundombinu ya kutolea huduma za haki.

Meya wa Manispaa ya Mpanda, Haidary Sumry, alisema Mkoa wa Katavi bado unakabiliwa na changamoto ya kuhudumiwa na jaji kutoka Mkoa wa Rukwa.

Hivyo, aliiomba serikali kutatua changamoto hiyo ili Mkoa wa Katavi upate jaji atakayeishi mkoani na kuwahudumia wananchi kwa ukaribu zaidi.

Wananchi waliohudhuria uzinduzi huo, waliishukuru serikali kwa kusogeza huduma za mahakama karibu kulinganishwa na awali walipokuwa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya nauli na mahitaji mengine.

Ujenzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi ulianza kutekelezwa Septemba 2017 na ulikamilika Julai 2021, ukigharimu Sh. milioni 652.



Nabii Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako ambaye ni Balozi wa Amani, Dk. Geordavie Kasambale, akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 50 kwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, Mrisho Gambo (kushoto), pamoja Ofisa Tarafa ya Themi, Chausiku Baha, kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wenye mitaji midogo na kurekebisha miundombinu ya soko la Samunge, jijini Arusha juzi. Nabii huyo, aliongeza Sh. milioni 50 nyingine na kufanya kuwa Sh. milioni 100. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Bosi Magereza aagiza kuimarishwa Kitengo cha Utunzaji Kumbukumbu

**Na Renatha Msungu** DODOMA

MKUU wa Jeshi la Magereza, Ramadhan Nyamka, ameagiza kuondolewa wafanyakazi wasio na uzoefu katika Kitengo cha Utunzaji Kumbukumbu ili kuepusha kuvuja kwa siri.

Pia ameagiza kuimarishwa mawasiliano baina yao ili kujenga tabia ya kufanya kazi kwa mawasiliano na si kila mmoja kufanya kivyake.

Aliagiza hayo juzi alipofungua mafunzo ya utunzaji kumbukumbu yaliyofanyika jijini Dodoma kwa siku mbili yakihusisha maofisa magereza nchini.

Alisema kuwa baada ya mafunzo hayo anahitaji kuona wataalamu watakaokaa kwenye kitengo hicho, wanakuwa na utaalamu wa kutosha katika kuhifadhi kumbukumbu.

Alisema hatosita kuchukua hatua kwa maofisa watakaobainika kuvujisha siri na kusababisha kukosekana umakini kwenye kitengo hicho muhimu. Aliwataka maofisa hao kuzingatia wanachofundishwa katika mafunzo hayo ili kuhakikisha wanakwenda kuwa watendaji wazuri kwenye utunzaji kumbukumbu.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuona askari wao wanakuwa na utaalamu wa utunzaji kumbukumbu na kuchangia kupunguza uvujaji siri.

Akizungumzia kuhusu mawasiliano kiutendaji, alisema ni jambo linalohitaji kufanyiwa kazi ili waende sawa na kazi wanazofanya.

Alisema kumekuwa na tabia ya kutokuwasiliana mahala pa kazi, jambo ambalo halitakiwi, akisisitiza mawasiliano yawepo ili uwelewano uwepo kazini.

Pia alizitaka ofisi zote za Jeshi la Magereza nchini ziweke wataalamu ambao ni wabobezi na wenye utaalamu ili kusaidia kutunza siri za serikali. Alisema wakuu wa vitengo hivyo wanapaswa 'kusema na jeshi' ili kuwapa wataalamu ambao ni wabobezi katika sekta hiyo.

Scholastika Ndunguru, Mkaguzi Msaidizi, alisema moja ya mafanikio ya Jeshi la Magereza ni kutengeneza wataalamu wazuri na wenye weledi.

Ndunguru alisema mafanikio hayo yanatokana na utendaji bora wa kazi ambazo jeshi hilo linafanya, hivyo baada ya mafunzo hayo wana imani wafanyakazi wa kitengo hicho wataimarika zaidi.

# Mgogoro AMCOS watikisa miradi uwekezaji katika Sekta ya Kilimo

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MGOGORO kati ya Bodi ya Chama cha Msingi cha Ushirika wa Kilimo na Masoko cha Machame Mkuu AMCOS na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro, unadaiwa kuathiri miradi ya kiuchumi ya wananchi wa vijiji viwili vya Nkuu Ndoo na Nkuu Sinde baada ya kusimamishwa kwa muda usiojulikana miradi ya uwekezaji wa kilimo cha migomba ya kisasa na kahawa vyenye thamani ya Sh. milioni 42.

Wananchi wa vijiji hivyo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Nkuu Ndoo, Twalibu Mallya, wamemwomba Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuingilia kati sakata hilo kwa kuunda timu maalum ya uchunguzi itakayohakiki miradi hiyo baada ya kuibuka madai ya ufujaji wa Sh. milioni 37 za chama hicho.

Juzi Mallya alisema: "Tunamwomba Waziri wa Kilimo (Bashe), Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu na Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe kufika Kata ya Machame Mashariki na kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huu ambao umemng'oa madarakani mwenyekiti wetu wa bodi na wajumbe wake katika mazingira ambayo tunaona kabisa uamuzi uliotumika umejaa ukakasi."

Alipotafutwa kuzungumzia mgogoro huo, Mwenyekiti wa Machame Mkuu AMCOS, Ibrahim Shoo, aliyeng'olewa na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro kwa madai ya kuwapo ubadhirifu wa fedha, alidai hakuna matumizi yoyote waliyoyafanya kwenye miradi hiyo bila wanachama kuhusika kuiidhinisha.

"Waliokuja na Mrajis Msaidizi wa Mkoa, walikuja na majibu yao na siyo kueleza wanachama shida iliyoko kwenye chama chetu.

"Pili, tunaona kuna shida, kwa sababu hao hao maofisa ushirika, ndio walikuwa wanajibu majibu ambayo walitakiwa kuvielekeza vyama vya msingi vya ushirika kabla na si kuja kutafuta matatizo.

"Tunajua kuna vyombo vinavyohusika na ukaguzi ambavyo serikali imeviunda kama COASCO. Sisi tulikwenda COASCO mwaka 2020, tukapata vitabu ambavyo vilikuwa vimetolewa quarrel (kasoro za ukaguzi) kuhusu ukaguzi uliofanyika wa miaka mitatu kuanzia 2017 hadi 2020.

"Wamekuja wanasema bodi inatakiwa isimame, wanasema bodi iliyoko ndiyo inabeba mambo yote. Wanachama wamehuzunika lakini wamelambishwa maneno ya mdomoni kwamba bodi hii mpya, ambayo imeanzisha miradi, imetumia fedha Sh. milioni 37 bila idhini ya Mrajis.

"Mimi nikiwa kama mwenyekiti, nimemweleza Mrajis kwamba hakuna matumizi yoyote tuliyofanya kwenye mradi huu, ambayo wanachama hawakuhusika kuudhinisha."

Chama hicho cha Machame Mkuu AMCOS kinamiliki shamba lenye ukubwa wa ekari 780, ambapo mwekezaji wa Kampuni ya Dekka Bruns anamiliki ekari 83 ambazo alikodishiwa na chama hicho. Mwekezaji mwingine wa Kampuni ya Bondeni Floweres anamiliki ekari 167.5 lakini ndani ya ekari hizo, ekari 25 alipewa na bodi iliyopita.

Kwa mujibu wa Shoo, mwekezaji wa Kampuni ya Makijaro anamiliki ekari 20 upande wa barabara ya Machame kuelekea njiapanda ya Moshi/Arusha na upande wa bondeni, anamiliki ekari 23 ambazo amekodishiwa kwa mkataba wa miaka mitano.

Aidha, Shoo alifafanua kuwa wanachama wa Machame Mkuu AMCOS wamebakia na ekari 200 ambazo zimegawanyika katika mafungu matatu.

# MAISHA

JANUARI 22, 2023
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 15

## Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako



Ukurasa 14

## Kuku wa limao



## SUTI ZA KUNG'AA


Ukurasa 13




# Limao linavyorudisha urembo

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

OGA, ALE, TOA, AKU, GOA, UZA UDA, PAA, AMBULIA, OA, AU, AITE, UANA, PUNGUZA

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA



MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kulima bustani ya mboga pembeni ya nyumba yao. Wakati wanalima Juma alimuuliza mama yake maana ya maneno aliyoambiwa na mwalimu wake.

Juma: Eti mama ni kweli mchuma janga hula na wakwao?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima watakula pamoja

Juma: Kwani ni lazima kila anayechuma janga lazima ale na ndugu zake?

Mama: Mwanangu huo ni msemo unaomaanisha kila baya unalolitafuta, utaathirika pamoja na ndugu zako ni lazima kujiepusha.

**SWALI**

Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Siri kuu mbili kuvuka mwaka huu 2023!

KARIBU tena msomaji wangu tumulike maisha yalivyo. Bado tupo kwenye vuguvugu la mwaka mpya. Wapo waliofanikisha mipango yao mwaka jana na wengine waliishia njiani. Yaani hawana cha kujivunia huku wakibaki na mawazo kwa nini hawakutimiza ndoto zao.

Kundi hili linashindwa kuelewa kwamba maisha ni siri. Na zipo siri mbili duniani; siri ya Mungu na siri ya shetani. Kila mtu anayo siri yake. Neno la Mungu linasema: “Siri ya BWANA ipo kwao wamchao, naye atawajulisha agano lake” (Zab.25:14).

Duniani kuna utawala wa Mungu na utawala wa shetani. Ndiyo maana nasema ziko siri mbili duniani. Siri ya Mungu hukaa kwa wale wamchao. Ukiona mtu amefanikiwa, ujue anaijua siri fulani. Ili ufanikiwe lazima uwe na siri. Mwaka huu 2023 lazima uwe na siri kuweza kutimiza ndoto yako!

Siri ya kwanza unayotakiwa uwe nayo ni maono. Pengine utauliza maono ni nini? Maoni ni picha ya mbele kule unakokwenda. Je, unakwenda wapi. Ni ile picha akilini mwako kuhusiana na kesho yako. Unaona nini mbele yako? Kile unachokiona ndicho utakachopokea.

Ukiona ushindi, utashinda, ukiona kushindwa, utashindwa kweli. Ukiona kuinuliwa au kubarikiwa ndivyo itakavyotokea. Hata ukiona kufa, utakufa kweli. Maoni pia ni dira ya maisha yako kesho. Jiulize mwaka huu unaona nini kwenye biashara. Unachokiona ndicho utakachopata. Hayo ndiyo maono!

Mwaka huu 2023 lazima uwe mtu wa maono. Ona kufanikiwa, afya njema, ushindi, kuinuliwa, ndoa nzuri, mahusiano mazuri. Mungu hawezi kukupa kitu ambacho hukioni. Ukiona kibaya ndicho kitakutokea.

Ndio maana mtu anaweza kusimama na kusema; mbona leo nakosa amani, sioni amani. Maana yake mabaya yanakuja! Mungu akamuuliza Nabii Amosi; “Unaona nini? Nikasema, naona timazi. Ndipo BWANA akasema, tazama nitaweka timazi kati ya watu wangu Israel...” Timazi yaweza kuwa uchungu, magonjwa, kilio, hasara na kadhalika.

Unachokiona utakipata na Mungu haendi zaidi ya maono yako! Pia Amosi 8:2 Mungu anamuuliza, Amosi unaona nini? Nikasema naona kikapu cha matunda wakati wa hari. Ndipo BWANA, akaniambia mwisho wao umewajia watu wangu Israel. Sitawapita tena kamwe”.

Hari ni wakati wa joto kali, ni hali ya ukame, hakuna vitu vinastawi. Mungu anaposema hatawapita tena kamwe manake watarajie mafanikio, furaha, faida na maisha mazuri. Mwaka huu haina maana hautakutana na majaribu, la hasha!

Majaribu ni wakati wa hari lakini kitakuwepo kikapu cha matunda. Ukiona mema yatakujia na ukiona mabaya kadhalika utayapata. Muombe Mungu akupe mema mwaka huu, yote yaliyoshindikana mwaka jana ayafanikishe.

Wako watu badala ya kujitafakari wao, huona wenzao wanashindwa. Kumbe hao wana maono kule waendako. Achana na wanaokuwazia mabaya. Wewe ona kuinuliwa, kufanikiwa kwenye kazi, biashara, mahusiano na kadhalika. Amini kile unachokiona mbele yako kufanikisha malengo yako! Mwambie Mungu akupe kuona vitu sahihi. Ukijiona mdogo, Mungu anakuona una kitu kikubwa ndani yako alichokuumbia!

Maisha ya mwanadamu yako mikononi mwake na siyo kwa mtu mwingine. Wapo watu wengine huhesabia wenzao miaka ya kuishi. Hao wanajifurahisha kwani hesabu za maisha ya mtu zipo mikononi mwa Mungu mwenyewe.

Mwaka huu anza kuona sasawasa. Ondoa macho ya makengeza, ona ushindi. Methali 29:18 neno la Mungu linasema, “Pasipo maono watu huacha kujizuia”. Wapo watu wanaojilaani wenyewe, wanajitamkia mabaya wenyewe hawajui wafanyeje.

Ni kweli kabisa kwamba changamoto ni sehemu ya maisha. Lakini unapomkimbilia Mungu kwa kushindwa kwako, Yeye kwake yote yanawezekana kuyakomesha.

Siri nyingine ni Nidhamu. Uwezo wa kutawala roho na nafsi, hiyo ni nidhamu. Jiulize je, una uwezo wa kutawala alichokupa Mungu? Yamkini Mungu aliwahi kukupa mikononi mwako kushika fedha nyingi hadi mamilioni. Leo yako wapi?

Si kila ulichopoteza alikupotezea shetani. Ni wewe huna nidhamu ya matumizi. Unamsingizia shetani hadi akaota mapembe, kumbe tatizo ni wewe huna nidhamu ya kutawala ulichonacho, umeshindwa kukimiliki!

Wako watu waliofanikiwa kushika mamilioni ya fedha na kuyapoteza leo hawayaoni tena, wanahangaika. Kumbuka tofauti kati ya tajiri na masikini ni uwezo wa kutawala mali.

***Msomaji wangu. Bila shaka hadi hapa umejifunza kitu kuhusu siri ya kufanikiwa. Tuma ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Acha kuinua mabega, kiburi ni anguko lako

KIBURI hutangulia kabla ya anguko la mtu. Chanzo cha kiburi mara nyingi ni mtu kujikweza na kujiona yeye ni bora kuliko wengine.

Nataka kusema nini? Ni hivi, migogoro mingi ya vyama vya ushirika nchini inayoendelea kuchipua hivi sasa, inasababishwa na kiburi ama viongozi kutunishiana msuli kutokana na maslahi binafsi au uvivu wa kujielekeza katika matakwa ya sheria na kufuata maadili ya kazi yake (code of conduct).

Nikiri wazi kwamba jitihada kubwa zinazofanywa na serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kufufua sekta ya ushirika, kuhimiza ustawi na uhimilivu wa vyama vya ushirika ili kuviwezesha kuwa vyenye nguvu na tija kubwa katika uzalishaji mali, zimerejesha matumaini ya kiuchumi ya wananchi walioamua kujiunga na vyama hivyo.

Januari 16, mwaka huu, kumeibuka mgogoro mpya, kati ya Bodi ya Chama cha Ushirika wa Mazao na Masoko cha Machame Nkuu AMCOS na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro, kutokana na uamuzi wenye ukakasi ulioing'oa madarakani bodi iliyoasisi miradi mikubwa miwili ya kilimo biashara cha kahawa na migomba ya kisasa.

Mgogoro huo unaathiri miradi hiyo ya kiuchumi, ambayo ingewanufaisha wanachama, ambao katika ekari 11 kati ya ekari 200 walizio nazo kwa sasa, wameweka kilimo biashara kwa kupanda miche mipya ya kisasa ya mibuni, na ekari nne wameweka miche ya migomba zaidi ya 4,000 na wakati huo huo katika eneo hilo hilo kuna miche 4,000 tayari imeshanunuliwa kwa ajili ya kupandwa shambani.

Yako mambo mawili yanayotajwa kama kiini cha mgogoro huu. Moja ni kuwekwa kabatini, makisio ya mradi wa shamba la migomba ya kisasa ya kimalindi, ambayo ilitengewa bajeti ya Sh. milioni 26 na makisio ya mradi wa kahawa za kisasa, uliokuwa umetengewa Sh. milioni 16.

Jambo la pili, ni tuhuma za ubadhirifu wa Sh. milioni 37 za chama hicho zinazodaiwa kutumika bila kibali cha Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro.

> **“Ushirika ni sekta muhimu yenye mchango mkubwa kwa taifa, ambayo inahusisha shughuli za uchumi ikiwamo kilimo na nyanja nyingine za uchumi ambazo zote hutoa ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.**

Madai ya kutumika mchakato haramu wa kuiondoa bodi kwa kutumia ripoti ya bodi nyingine iliyopita ni makosa. Kama kuna hoja za ukaguzi wapeni kazi, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini (COASCO) na sio kuteua maofisa ushirika kufanya ukaguzi. Kama ni suala la ubadhirifu ziko hatua zinapaswa kuchukuliwa ikiwamo kuisimamisha kazi bodi na kuiburuza kortini kwa tuhuma zinazowakabili lakini kuifukuza peke yake.

Nasema hivyo kwa sababu, mara kadhaa tumeshuhudia, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisema serikali ina mkakati wa kuendeleza na kuimarisha ushirika, kwa kuanzisha na kufufua viwanda ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa na wanaushirika.

Ni dhahiri kuwa Waziri Mkuu Majaliwa, amekuwa jicho la karibu la vyama hivi, kwa kuagiza mara kwa mara Wizara ya Kilimo isimamie kikamilifu matatizo mbalimbali yanayodumaza vyama vya ushirika nchini ili kujenga ushirika imara unaokuwa na endelevu. Haya ndiyo mambo ya kufanyia kazi na si baadhi ya watendaji kujisahau.

Pia Waziri Mkuu, Majaliwa amekuwa akisema serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kuwa vyama vya ushirika vinaimarika na wakulima wanapata tija ya manufaa ya shughuli za uchumi zinazoendeshwa kwenye vyama vya ushirika.

Ushirika ni sekta muhimu yenye mchango mkubwa kwa taifa, ambayo inahusisha shughuli za uchumi ikiwamo kilimo na nyanja nyingine za uchumi ambazo zote hutoa ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

Na ninyi viongozi na watendaji wa sekta ya ushirika ni lazima mhakikishe kuwa vyama vya ushirika vinaendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu na kusimamia vyama kwa misingi ya uadilifu ili kuondokana na matatizo ambayo yamekuwa yakiharibu taswira ya ushirika.

Tuache kuinua mabega, tukae turidhiane, kiburi ni daraja la anguko lako!

- ***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com, Simu ya mkononi: +255 767 535490***











Desemba 30, 2022 ilikuwa siku ya furaha kwa Gaudin Gration alipofunga ndoa takatifu na Bibiana Deus, katika Kanisa Katoliki la Katoke wilayani Muleba mkoani Kagera na baadaye kuwa na tafrija fupi iliyofanyika ukumbi wa Suzana.

# MITINDO





## SUTI ZA KUNG'AA

MWAKA 2023 ni wakati wa kuvaa mavazi adimu yenye mng'aro wa kuvutia.

Baadhi ya wabunifu wameutaja mwaka huu kuwa ni wenye mafanikio katika mitindo ya mavazi na rangi zenye kung'aa.

Tofauti na mwaka jana uliotawaliwa na rangi hafifu, mwaka huu ni mwendo wa kujing'arisha zaidi kwa suti kali zinazomfanya mtumiaji kuwa wa kipekee.

Rangi kama nyekundu, bluu, manjano ya limao, kijani ya kiwichi, nyeupe na kijivu zinapendekezwa kutawala zaidi kwa misimu yote ya mwaka.

Unaweza kusema ni kipindi cha vijana kutawala zaidi kuliko wale wenye umri wa kati na zaidi. Vijana wengi wanapenda vitu vyenye mng'ao na hata kwenye mavazi wanapenda kuwa katika hali hiyo.

Wabunifu wa mavazi watakuwa na msimu mzuri wa kujipatia kipato kutokana na kuwa na kazi nyingi zaidi kuliko kipindi cha nyuma.

Rangi huongozwa na vivuli vya pastel, ikiwa ni pamoja na rangi nyekundu, peach, cream, HYPERLINK "https://confettissimo.com/sw/Goto/https%3A/womanadvice.ru/Cvetslonovoy-kosti-na-kakoy-ni-chemsochetaetsya-v-odezhde" \t "_blank" Ivory champagne na nyeupe za jadi, zinazohusishwa na wanawake wadogo wenye huruma, hatia na vijana. Wakati huo huo, katika makusanyo ya mtindo maarufu wa mtindo, bidhaa zote nyekundu zenye chaguzi za kawaida katika tani za mint zinawasilishwa.

URЕМBO

Na Mary Geofrey

# Limao linavyorudisha urembo



NGOZI kwa kawaida inatakiwa ijitengeneze yenyewe na si kuitengeneza kwa kutumia vipodozi kama wengi wanavyodhani.

Ulaji wa matunda na mboga za majani kwa wingi kunywa glasi nane za maji kwa siku, ni njia nzuri kama unataka kuwa na ngozi nzuri isiyo na madoa wala ukavu ambao haupendezi.

Wengi wanaacha kula mbogamboga na matunda kwa wingi hata kutokunywa maji ya kutosha, badala yake wamekuwa akitegemea kuwa na ngozi nzuri jambo ambalo ni gumu.

Mara kadhaa tumeshuhudia watu wanaopaka krimu kali wakiwa kama wameungua usoni, huku mwili ukionekana kuwa mkavu jambo ambalo linaashiria kuwa krimu si suluhisho la kuwa na ngozi nzuri.

Kuna watu wamekuwa na ngozi za asili na hata unapowauliza baadhi yao hawajawahi kupaka cream hata siku moja na bado wana ngozi nzuri zinazovutia hao wamekuwa wakila kwa ajili ya kuhakikisha wanatengeneza ngozi zao kutoka ndani.

Wengi wanaharibu ngozi zao na kuwa na madoa kutokana na kutumia make up kwa muda mrefu na hata anapogundua kuwa ana tatizo la madoa.

Wamekuwa wakijaribu kutumia vipodozi vingine kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo jambo ambali linazidisha madhara kwenye ngozi.

Unaweza kutibu ngozi yenye madoa usoni pia mashavuni kwa kujitibu na juisi ya limao.

**NAMNA YA KUFANYA**

Chukua limao lioshe na kisha likamue na kuchuja mbegu zake. Weka juisi hiyo kwenye kikombe na kisha tafuta kitambaa laini kichovye kwenye juisi ya limao na dondoshea juisi ya limao kwenye sehemu zenye tatizo.

Kaa kama dakika tano kisha osha uso kwa maji safi. Unaweza kuchanganya na asali mbichi na maji ya limao husaidia pia kuondoa madoa usoni.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kuku wa limao



KUKU ni chakula kizuri kwa familia. Kama unahitaji kujilamba na kuvinjari, basi kula kuku wa limao.

Jinsi ya kuandaa

Changanya viungo kwenye blenda, saga ili upate mchanganyiko mzuri na hifadhi pembeni.

Andaa kuku, unaweza kumkata vipande au ukamuacha mzima kisha msafishe na mkaushe kwa kitambaa safi.

Kama unataka kuoka kuku, hakikisha kuwa huondoi ngozi. Ngozi husaidia kumfanya kuku aive vizuri sababu inaungua huku ikiacha nyama ya ndani ikiiva vizuri na taratibu.

Kwenye mfuko wa plastiki weka mchanganyiko wa viungo vyote, kisha weka kuku na umchanganye vizuri ili apate kuingia viungo.

Hifadhi mfuko wenye kuku kwenye friji kwa takribani saa sita hadi saba ili vipikwe kesho yake.

Ukiwa tayari kuandaa kuku, toa kwenye mfuko, panga kwenye bakuli akauke kwenye oven.

Washa oveni na uipashe moto kwenye nyuzi joto 150, halafu kamua limao kwenye chombo kikavu. Changanya maji ya limao na mafuta ya kula kwa pamoja upate mchanganyiko sawia.

Kata vizuri vipande vya limao lililobaki na weka pembeni, usitupe.

Mwaga mchanganyiko juu ya vipande vya kuku vizuri. Mloanishe ili apate kuwa na unyevunyevu mzuri.

Panga vipande vya limao kwenye bakuli vizuri pembeni ya vipande vya kuku.

Washa oveni kwa dakika 45 na weka kuku ili apate kuiva. Unaweza kuangalia kama anaungua ili kumgeuza.

Baada ya dakika 45, toa kuku na angalia kama ameiva vizuri ndani.

Unaweza kula chakula hiki na ugali, wali, ndizi au vinginevyo.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako

UZIO ni moja ya sura ambazo zinaweza kutumika kama urembo wa nyumba kulingana na namna mhusika anavyotaka. Mwenye nyumba anaweza kutaka uzio huo uwe kwa kutegemea bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla, nyumba inapozungushiwa uzio, iwe ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au mwonekano, unasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba husika.

Kwa mazingira yetu ya kitanzania, kuna uzio wa aina mbalimbali ikiwamo za matofali, mbao, miti, makuti, chuma, wavu na mabati.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Michael Samuel, anasema yako mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba yako.

Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa, kuna uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadaye. Kwa hiyo mbao zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu pasipo kufanya hivyo zinaharibika. Hivi ni vitu ambavyo unapaswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka," anasema Samuel.

Jambo lingine, anasema kabla ya kutengeneza uzio wako, unatakiwa ufahamu unatakiwa uwe kwa mtindo gani. Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi unasaidia kuweka mwonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Samuel anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na siyo bora uzio.

Anasema uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba, hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha bali ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.



## Namna ya kupamba kwa michoro



Michoro ya ukutani inayoweza kutumia kupendezesha nyumba.

Kama mpenzi wa michoro ya kiafrika, basi unaweza kupendezesha kuta za nyumba yako kwa sanaa za Kitanzania.

Hata hivyo, unatakiwa kuwa na ufahamu wa aina ya michoro unayotakaa kuweka ndani ya nyumba, na hizi ni baadhi ya dondoo za michoro inayoendwa.

**1I Tingatinga**

Tingatinga ni aina ya michoro ambayo ilianzia Dar es Salaam, kwenye karne ya 20 na baadaye ikasambaaa Afrika Mashariki nzima. Mwanzilishi wa michoro hii ni Edward Saidi Tingatinga.

**2: Michoro ya kisu**

Michoro hii ni ya kupendezesha nyumba ukutani kama ilivyo kwa ile ya tingatinga. Tofauti yake ni kwamba michoro ya kisu inaonyesha picha halisi.

**3: Michoro ya Zanzibar**

Kama jina lake lilivyo ni kwamba michoro hii inaakisi mwonekano wa mandhari ya Zanzibar kama vile ni milango, ufukwe na majengo mbalimbali ya Zanzibar.

**4: Michoro ya kanvasi**

Michoro ya kanvasi ipo ya aina mbili ambapo aina ya kwanza ni ile iliyoko kwenye kanvasi na ikakamilika. Aina ya pili ni ile iliyopo kwenye kanvasi zaidi ya moja ili kuufanya mchoro mzima ukamilike. Kanvasi hizo zinaweza kuwa tatu au nne na ukiondoa moja mchoro wote unapoteza maana.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
NIMELIFUMANIA NA MKE WANGU LILIVYOKUWA BWEGE LIKANIPA HELA!
TWENDE TUKAMDISKASI BAR
JUKWAANI
!
KIOO. NGODH!
FUMUKO LA BEI
UNAMNUNIA NANI KWANI ULIVYOPANDA HUKULIONA KAMA LIMEJAA SANA?
NDIO UNIKA-NYAGE KWENYE MOKASINI?
LALAMIKA KAKA! MWENYEWE UME-PIGA KIWI ALAFU YEYE ANACHAFUA KIULAINI HIVYO?
DUH!
ACHA UJINGA KWA MOKA GANI HASWA?
MTAJUAJE KAMA ANA MOKA MPYA!
UNATAJA MILIONI MBONA UFANANI NA HIYO HELA?
MBONA UFANANI NA UBAHILI?
POMBE NA HELA ZA LIDANDASI NI MAPACHA
TOKA KAONDOKA
SUBIRI AFIKE MBALI
SMOLU HAUSI
NITAKU....!
WEEEE! NIKIPIGWA KAMA NIMEPIGA NA SIJAPIGWA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
UKIONA YUPO KIMYA USIMLAZIMISHE KUONGEA...

# Zelensky aomba vifaru haraka, Ujerumani yasita kutoa Leopard

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amesema hakuna njia mbadala kwa nchi za Magharibi bali ni kuipa Ukraine silaha nzito.

Hata hivyo mpaka jana Ujerumani ilishindwa kuthibitisha iwapo itatoa vifaru vyake chapa ya Leopards.

Mkutano ulioongozwa na Marekani uliwahusisha washirika takriban 50 wa Ukraine, umepitisha msaada wa kijeshi wenye thamani ya mabilioni ya dola, ikiwa ni pamoja na magari ya kivita na silaha zinazohitajika kurudisha nyuma vikosi vya Russia kwenye uwanja wa mapambano.

Hata hivyo Rais Zelensky, katika mkutano huo alisisitiza anahitaji zaidi vifaru vya kivita.

Akihutubia mkutano huo kwa njia ya video, Zelensky aliwahimiza washirika wake kuharakisha upelekwaji wa silaha na kuweka mkazo upatikanaji wa vifaru chapa ya Leopard 2, kutoka Ujerumani.

"Kila siku tunaona kwamba hakuna mbadala, zaidi ya kufanya maamuzi kuhusu upatikanaji wa vifaru," alisema Zelensky.

Matarajio yaliongezeka kwa washirika wa Ukraine, kabla ya mkutano huo uliofanyika siku ya Ijumaa.

Ilitegemewa Ujerumani kama ingelikubali ombi hilo, nchi zingine zinazotumia aina hiyo ya vifaru aina ya Leopard, wangeruhusiwa kuvipeleka Ukraine.

Sababu za Ujerumani kusita kutoa majibu ya moja kwa moja bado hazijawa wazi, kwani Uingereza imekubali kutuma vifaru vyake 14 aina ya Challenger 2 nchini Ukraine.

Hata hivyo, Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, alisema Ukraine inatarajiwa kufanya mashambulizi dhidi ya vikosi vya Russia katika wiki zijazo.

"Tunayo fursa kwa sasa na majira ya masika, wakati wowote watapoanza mashambulizi yao," alisema waziri wa huyo wa ulinzi wa Marekani.

Waziri wa Ulinzi wa Ujerumani, Boris Pistorius, aliwaambia waandishi wa habari kuwa bado hawawezi kusema ni lini uamuzi utachukuliwa na uamuzi utakuwa upi, linapokuja suala la vifaru vya chapa Leopard.

Austin aliitetea Ujerumani dhidi ya ukosoaji kwamba haikuwa ikifanya vya kutosha kuisaidia Ukraine, akisema serikali yake imekuwa mshirika wa kutegemewa.

"Sote tunaweza kufanya zaidi, Ujerumani ni mshirika wa kutegemewa.""

Alisisitiza Austin. Maofisa wa Marekani walisema Ukraine bado inakabiliwa na vita kali dhidi ya majeshi ya Russia, ambayo bado yanashikilia moja ya tano ya nchi hiyo.

Jenerali Mark Milley ambaye ni mkuu wa majeshi ya Marekani, alieleza kiwango cha vifaa vinavyohitaji, ikiwa ni pamoja na magari ya kijeshi, silaha pamoja na mafunzo kwa vikosi vya Ukraine.

Hata hivyo, Russia imeonya kwamba vifaru vya washirika wa magharibi kupelekwa Ukraine kutasababisha hali kuwa ngumu zaidi.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, alisema hoja hiyo haipaswi kupewa uzito mkubwa.

"Tunaona ufuasi wa udanganyifu mkubwa juu ya uwezekano wa Ukraine kuwa na mafanikio kwenye uwanja wa vita," alisema Peskov mbele ya wanahabari.

Alionya kwamba utolewaji wa misaada hiyo utaongeza tatizo zaidi kwa Ukraine, lakini haitabadilisha kitu kwa vikosi vyake katika kusonga mbele kwenye uwanja wa vita, kufikia malengo yake.

"Hii itaongeza matatizo kwa Ukraine, lakini kwa upande wa Russia haitabadili chochote katika kufikia malengo yake," alisema.

**HALI ILIVYO**

Wizara ya Ulinzi Russia, ilisema vikosi vyake vimechukua udhibiti wa eneo la Klishchiivka, ambalo ni makazi ya kusini mwa mji wa Bakhmut katika eneo la kimkakati la Donesk Mashariki mwa Ukraine. Wiki iliyopita, vikosi vya Russia vilitaja kuuteka mji wa Soledar ulioko Kaskazini Mashariki mwa Bakhmut.

Hatua hiyo inayotajwa na wachambuzi wa masuala ya ulinzi kuwa inaweza kuwasaidia kuweka shinikizo kwa mji mkubwa.

Mji huo uliokuwa na wakazi 400 kabla ya vita, ulitekwa kwa msaada wa mashambulizi ya anga.

Hata hivyo taarifa hizo hazijathibitishwa na mamlaka ya Ukraine kutoka katika uwanja wa vita.

**DW**



Makuhani wakuu wa dini ya Orthodox wakisherehekea sikukuu ya ubatizo kwenye Ziwa Batu nchini Ethiopia. Sherehe hizo hufanyika Januari 18 kila mwaka. **PICHA: AFP**

# Mshauri wa rais apelekwa gerezani

**KINSHASA,** DRC

MSHAURI wa zamani wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Fortunat Biselele, ambaye aliondolewa katika baraza la mawaziri wiki iliyopita, amepelekwa gereza kuu mjini Kinshasa.

Biselele ambaye alikuwa na ushawishi mkubwa kwa Rais Felix Tshisekedi, alihamishiwa kwenye gereza kuu la Makala jana usiku, baada ya kesi yake kusikilizwa kwa saa sita na waendesha mashtaka.

Biselele aliondolewa katika baraza la mawaziri Januari 14 na kuwekwa kizuizini.

Hata hivyo, sababu za kukamatwa kwake bado hazijajulikana. Taarifa iliyochapishwa na jarida la habari la Africa Intelligence, ilidai kuwa anashukiwa kushirikiana na serikali ya Rwanda.

Jarida hilo liliripoti kwamba Biselele alikuwa amejaribu kuileta DRC karibu zaidi na Kigali mwanzoni mwa utawala wa Tshisekedi.

**DW**

# Burkina Faso yawakomboa wanawake, watoto 66

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

JESHI la Burkina Faso limefanikiwa kuwakomboa wanawake na watoto 66 ambao walitekwa nyara mwezi huu na wanamgambo wa Kiislamu. Tukio hilo la utekaji lilitokea kaskazini mwa nchi hiyo wakati wanawake na watoto walipokuwa wakikusanya matunda mwitu karibu na mji wa Arbinda kwenye jimbo la Soum mnamo Januari 12 na 13.

Taarifa zilizotolewa jana na shirika la utangazaji la taifa RTB, zilisema kwamba vikosi vya usalama viliweza kugundua walipo mateka wakati wa operesheni zake kwenye mkoa wa Kaskazini.

Mji wa Arbinda umekuwa chini ya vizuizi vya wanamgambo kwa miaka mingi na hivyo kuwafanya wanawake na watoto kuwa katika hatari ya mashambulizi.

Wanamgambo hao wameizingira miji katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi na kutatiza usambazaji wa bidhaa na watu kutembea kwa uhuru.

**DW**

MAKALA

# MABADILIKO YA SHERIA NA KANUNI NI MUHIMU KATIKA HILI



Na Magabilo Masambu

JANUARI 3, mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kama lilivyo jina lake, alileta suluhu ya mikutano ya vyama vya siasa nchini ambayo ilipigwa marufuku na mtangulizi wake, Hayati John Magufuli, takribani miaka saba iliyopita. Suluhu hii imekuja baada ya mazungumzo kati ya Rais na viongozi wa vyama vingine vya siasa.

"Kwa hiyo uwepo wangu leo mbele yenu ni kuja kutoa ruhusa. Kuja kutangaza kwamba, lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara limeondoshwa." Hii ni kauli ya Rais katika kikao na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajili uliofanyika Ikulu, Dar es Salaam.

Kwanza, niungane na wengi ambao wameupongeza uamzi huo wa busara, ambao umefanywa na Rais kupitia majadiliano ya muda mrefu kidogo pamoja na viongozi hao. Pia niwapongeze viongozi wa vyama hivyo ambao walishiriki mazungumzo hayo na kuwezesha kupatikana kwa suluhu hiyo. Pamoja na kufunguliwa huko ni muhimu kwenda mbali zaidi.

Aliyetoa tangazo la kufungia mikutano ambayo ipo kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya Vyama vya Siasa ni Rais wa Tanzania na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) awamu ya tano na tulishangilia. Aliyefungulia na kufuta katazo hilo ni Rais wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM na tumeshangilia vilevile!

Tafsiri rahisi ni kwamba kuna uwezekano mkubwa bado mikutano ya vyama vya siasa ikazuiwa huko mbele. Kama si awamu ya sita tunaweza kumpata Rais mwingine ambaye pengine hatakuwa mwema kama alivyo Rais Samia leo. Rais wakati akiondoa katazo hilo, alisema ni haki kwa vyama vya siasa kufanya mikutano, maana yake haki hiyo inatokana na sheria tulizo nazo nilizozitaja hapo juu lakini bado hazikufuatwa.

Maana yake ni kwamba pamoja na vyama kuruhusiwa kufanya mikutano na kama alivyosema Rais kwamba serikali na chama kinachotawala wako tayari kukosolewa, lakini uhuru watakaokuwa nao katika kufanya mikutano itakuwa kama mtu aliyekufungia ndani ya nyumba yake, akaamua kukufungulia kutoka ndani ya nyumba lakini unapofika nje, unakutana na ukuta wenye geti. Yaani unakuwa nje ya nyumba lakini ndani ya geti la nyumba hiyo kwa sababu aliyekuruhusu uongee ndiye atakayekuwa anapima maneno unayoyasema juu yake. Kwa mantiki hiyo, bado anao uwezo wa kusema bwanae umenisema sana, sasa nafikiri uishie hapo.

Nadhani, kama tunakubaliana kwamba nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa Katiba na sheria, basi ni muhimu kulinda viapo vyetu kama ambavyo Rais Samia ameamua kulinda kiapo chake cha kusimamia Katiba na sheria. Hapa kuna Katiba ya nchi, Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Sheria ya Jeshi la Polisi dhidi ya mikutano hiyo. Kwa maana hiyo ni imani yangu kuwa hatazuia tena mikutano, kwa sababu ni muumini wa Katiba na uamuzi huo amefanya kwa mujibu wa Katiba. Kama tunaona sheria zetu zina upungufu, sote kwa pamoja tukubaliane kufanya marekebisho ili asitokee mtu akasema nimezuia na ikiwa atafanya hivyo, ashtakiwe kwa mujibu wa sheria.

Vyama vingi vya siasa vina umuhimu sana kwenye nchi si kwa ajili ya kuharakisha maendeleo tu, bali vinakiwezesha chama kilichoko madarakani kujisahihisha na katika kujisahihisha huko, ndio uhai wa chama hicho. Mikutano ya vyama itasaidia kusema wapi chama tawala kinakosea na ikiwa kitarekebisha makosa hayo, maana yake kitaendelea kuwa madarakani.

Lakini kushindana kwa hoja kutajenga watu imara ndani ya vyama vyote. Watu hawatakuwa waoga wa kujenga hoja na kujibu maswali ya wananchi. Kutokuwa na mikutano wala majadiliano, kunawafanya wale wanaojiita wanasiasa kutokuwa na uwezo mkubwa wa kukabiliana na hoja za watu. Viongozi wengi wa kisiasa ambao kazi yao kubwa ni kuongea bado wanaogopa kuulizwa maswali na waandishi wa habari.

Ni jambo la ovyo sana viongozi au kiongozi anaitisha mkutano wa waandishi wa habari anahutubia haraka haraka kisha anafunga mkutano na hataki kuulizwa maswali. Imetokea mara nyingi hata juzijuzi viongozi fulani waliitisha mkutano wa waandishi wa habari wakaruhusu swali moja! Hii ni moja ya madhara ya kuzuia mikutano ya kisiasa. Uwezo wa viongozi kujieleza unakuwa mdogo, hivyo wanabaki kusifiana na kupongezana tu. Hili nalo limefifisha uwezo wa wengi na yeyote anayekimbia maswali ni mhalifu.

Mabadiliko ya sheria yakifanywa kwa nia njema, yatamsaidia kila mtu ndani ya nchi. Mkipata Rais asiyeheshimu Katiba na sheria, ndipo mtagundua kwamba kumbe athari zinampata kila mtu na kupitia uongozi fulani uliopita huko duniani, ungetupatia funzo la kukubaliana kwa pamoja namna bora ya kudhibiti viongozi wa aina hiyo. Tukiendelea kuongozwa kwa busara za Rais anayekuwa madarakani, halafu naye ni mtu kama wengine, basi kuna siku taifa hili litaingia kwenye matatizo makubwa na hatutakuwa na uwezo kufanya lolote. Mwenye macho haambiwi tazama.

Uhai wa vyama vya siasa unapaswa kuwa wa kisheria, hivyo ulindwe na uheshimiwe. Uhuru huo ukiwa unatumia busara za mtu, tutakuwa tunakwenda hata 10 mbele kisha tunarudi hatua tisa. Sisi sote ni mashuhuda wakati wa Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, ndio pekee kwenye historia ya nchi hii, wanasiasa wengi vijana walionekana na kuanza kushiriki katika siasa. Bunge likawa na mvuto, kwa sababu huko nyuma ilionekana siasa ni za wazee. Haya yalifanyika kwa sababu kulikuwa na huru mkubwa wa kufanya shughuli za kisiasa pamoja na uhuru wa kujieleza.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Baharia aliyerejea Bongo, mkewe hayupo kamtoroka*



Na Adam Fungamwango

MAISHA yana changamoto kubwa sana na hayajawahi kunyooka hata siku moja kwa masikini na matajiri. Mbaraka Mwinshehe Mwaruka alimaliza kila kitu alipotunga kibao cha 'Shida' mwaka 1978.

Kwenye mashairi yake aliimba: "Hakuna kitu kibaya sana duniani kama shida. Haichagui siku shida wala mwaka, haina katu taarifa shida huingia shida bila hodi. Si mtoto wala mkubwa wote shida. Kila siku shida shida, haishi mpaka siku ya mwisho.

"Shida haikosekani hata kama siku ya harusi na uwe na mapesa mengi ipo shida. Haina ngoja wala aibu popote shida hutokeza. Kwa masikini matajiri wote shida, kila siku shida shida haishi mpaka siku ya mwisho."

Ni wimbo ambao haukuwa na mashairi mengi sana, lakini haya machache yameshiba na kudhihirisha kile ambacho alitaka kukiongea na kipo kwenye jamii yetu.

Mbaraka anasema ukiwa na pesa shida ipo tu. Ukiwa huna pesa ndiyo kabisa yaani shida hapo ndiyo kama nyumbani kwake.

Mtunzi alikuwa anaeleza kuhusu kitu shida ambayo kwa sasa wengi wameenda mbali sana na kuiita changamoto. Lakini hiyo ni shida au matatizo na unaweza kusema tabu vile vile.

Mbaraka anasema siku zote shida haipigi hodi, inatokea tu ghafla na wala huwezi kujua imetokea wapi. Maana yake binadamu hajipangi kwa ajili ya kukabiliana na shida, bali shida huja kwanza na yeye anaanza kuitatua kwa sababu haipigi hodi.

Halafu anasema popote pale inatokea. Ngoja na mimi nimuunge mkono na kumuongezea Mbaraka kitu. Shida hutokea popote pale, iwe mjini, kijiji, porini kwenye usafiri hata kwenye sehemu ambazo hatu hufurahi, lakini kikubwa zaidi hupenda kutokea sehemu ambayo ni muhimu au nyeti sana kwa mhusika.

Kama umevaa ndala, mara nyingi hukatika mbele za watu. Unaendesha gari, pikipiki au basikeli, huharibika sehemu ambayo kuna watu wengi ambao hawakupendi au wanakuonea kijicho, ili tu wapate na kuongea.

Au ukaanguka mbele ya msichana au mvulana unayempenda ambaye labda juzi tu ndiyo mmetoka kuzungumza masuala ya mapenzi. Ndiyo maana waswahili wakawa na msemo wao mmoja kuwa 'siku ya kutembea utupu ndiyo siku ya kukutana na mkweo.'

Maana na msemo huu kuwa siku ambayo wewe hujajiandaa na lolote lile, au kuchukua tahadhari yoyote, ndiyo siku ambayo kuna kitu kitakutokea ambacho kwa wakati huo utashindwa kabisa kukitatua.

Mbaraka anasema shida ipo tu hata siku ya harusi. Yaani changamoto inaweza kutokea hata siku ambayo watu wana furaha.

Mfano tu, siku hiyo vyakula au vinywaji vikaisha wakati bado wahudhuriaji na wengi bado hawajapata, kukazua malalamiko na mzozo.

Kwenye maisha haya, kila mmoja ana kazi yake ambayo pia ina changamoto zake. Kuna kazi ngumu sana, na zipo zenye kutumia zaidi akili mpaka mtu anakuwa kama amechanganyikiwa. Kuna kazi zisizo na mapumziko ya Jumamosi, Jumapili au sikukuu.

Pia zipo kazi ambazo mtu akitoka nyumbani kwake leo, kurejea kama itakuwa ni mapema sana basi ni miezi mitatu.

Hao ni pamoja na madereva wa malori. Kuna rafiki yangu mmoja aliwani kunichekesha, lakini pia ndani yake kukiwa na ujumbe uliofika vema kwenye hadhira.

"Ndugu yangu, hii kazi yetu ya madereva malori kama huna mke mwaminifu unaaweza kupata mwanaume mwingine wakawa wapenzi kwa muda mrefu hadi wakagombana na kuachana wewe hujui."

Ujumbe wake hapo ulikuwa ni kwamba aina ya kazi yake haimpi fursa sana ya kukaa na familia yake, kwa sababu akirejea nchini anaweza kukaa wiki moja tu au mbili, lakini akiondoka kwenda nchi za nje kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Zambia, Rwanda au Burundi ni miezi mitatu.

Yote tisa, kuna kazi ya ubaharia hasa ya meli zinazokwenda nje ya nchi. Mtu anaweza kukaa miezi sita, mwaka au zaidi hajarudi nyumbani. Kuna mtu alishawahi kuniambia kuwa zamani mabaharia ilikuwa ni mara chache sana kuoa na kuwa na familia kwa sababu hiyo.

Kwa sasa mambo yamebadika, lakini inahitaji kuwa na familia yenye msimamo na inayojua asili ya kazi ya baba yao. Baadhi ya mabaharia waliokuwa akiondoka na kuwaacha wapenzi au wake zao, hawakuwakuta kwa sababu walishindwa kuwavumilia kukaa kipindi chote hicho, wakawakimbia kwenda kuolewa na watu wengine.

Mwanamuziki Kasongo Mpinda Clyton alipata kisa hiki na kukitungia wimbo aliouita 'Kazi yangu Baharia' akiwa na bendi ya Maquis Original.

"Mimi kazi yangu baharia, mwaka mmoja au miwili kazi ya bahari. Nakubali shida na matatizo. Yote hii ni kwa ajili ya watoto wangu. Yote hii juu ya kujenga familia yangu ee. Likizo napata narudi nyumbani, nakuta mama watoto ametoroka jamani ee. Ningine nadni ya nyumba yangu, naona giza. Nitoke nje nitazame juu, naona jua na mwezi vinakutana leo. Mama nalia eee, mizimu ya mababu, njoo, mimi naumia, oo yele naumia.

Kumwacha mke wangu, nashindwa kweli mama, watoto kuwalea na mama wa kambo siwezi kweli mama. Malezi mema ya watoto ni kuwalea baba na mama yoyo.

Nakwenda zangu safarini tuliangana salama naye, ahadi tukapeana mashahidi malaika mama. Nilimwamini leo yeye kanigeuka tena, mizimu ya mababu sijui la kufanya kweli.

Maungo yamenilegea juu yake yeye na kazi bado kwisha sijui nitafanya nini yoyo."

Hizi zote ni changamoto za maisha. Lakini pamoja na hayo haziwezi kumfanya mwanaume aache kufanya kazi kwa sababu eti iwe na familia yake kwa muda mrefu.

TX Moshi William aliimba wanaume tumeumbwa mateso kuhangaika. Usiache kazi fulani ambao umeandikiwa eti kwa sababu inakufanya uwe mbali na familia. Kwa sababu kinakukuta kitu kikubwa zaidi ya hicho.Kwa sababu hata hiyo familia inahitaji kazi yako ili ipate mahitaji yake, iwe na amani na furaha.


**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Harusi imevunjika-15

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




BWANA ee, kweli nimekimbia harusi yangu mwenyewe, lakini mimi nilifuata pesa na maisha mazuri kwa Jaziru, ila Jerry ndiyo yupo moyoni mwangu."

"Eeeeh dada we, uliyemkimbia siku ya harusi kabla ya ndoa haijapita..." Akaongea Nasma kama kwa kejeli hivi.

"Maisha ndugu yangu. Si nimekwambia ile kukimbia tu hapa ilikuwa ameshaniingizia shilingi milioni saba, na Zulfa alivyolazwa nilipopata taarifa nikamdanganya kuwa mama yangu amelazwa nataka nitume nyumbani akanipa shilingi milioni tatu. Hata hapa nilipo kakamatwa tu lakini tayari kwenye akaunti yangu kuna shilingi milioni 10. Biashara yoyote ile sasa hivi naweza nikaifanya, hivi sasa nimetuliza kichwa tu kwanza ili nijue nitafanya nini."

"Jerry umeshaonana naye?"

"Mwenzangu hilo ndilo linaloniumiza kichwa."

"Vayajo, na aibu ile uliyompa baba wa watu unadhani unaweza kweli?"

"Unajua shoga yangu, hakuna mkate mgumu mbele ya chai. Yule Jerry nikikaa naye naye, nikalia, nikambembeleza, nikamuomba radhi, tena nikimwambia nina shilingi milioni kumi benki tuanzishe biashara au mradi wowote, sijui kama atakataa."

"Mmmh, inawezekana mwaya."

"Ila dada we, kuna kitu kimeingia kati hapa, naona kama itakuwa kazi kubwa kushawishi mpaka kukubali. Isingekuwa hivyo kazi yangu ingekuwa rahisi tu."

"kitu gani hicho?"

"Huyu ndugu yangu."

"Ndugu yako yupi tena dada wewe?"

"Zulfa."

"Zulfa?"

"Unashangaa tena."

"Ndiyo, lazima nishangae Vayajo, unaniambia Zulfa, halafu zijakuelewa ati."

"Zulfa anaonekana kama ameshanipiga bao kwa Jerry."

Nasma alipiga makofi dhaifu ya mshangao. Halafu akaweka mkono mmoja shavuni akamalizia kwa kusema.

"Toba, Zulfa huyu huyu ndugu yako?"

"Huyu huyu unayemjua wewe Naa shoga yangu, mtoto kanikalia kooni huyo."

"Niambie koma we. Yameanza lini tena mapenzi hayo?"

"We acha tu, si tangu alivyoumwa. Si alikaa kule miezi kama mitatu hivi. Ulimuona wewe alivyorudi?"

"Jamani mdogo wako si alikuwa anaumwa kaka wa watu kajitolea kumuuguza na kumgharamia, leo tena kawa mpenzi wake eee."

"We Naa wewe, we hujui, Zufla karudi kanawiri, kapendeza utadhani katoka Sauzi au Ulaya, yaazni huwezi kudhani kama alikuwa anaumwa. Kila mtu akawa anamshangaa. Mama kanipita uzuri mpaka mimi dada yake. Iliona zile nywele alizosuka? Iliona ngozi yake ilivyozidi kuwa nyororo? Uliona nguo zake za gharama? Uliona nguo zake alizorudi nazo? Yaani ukae miezi mitatu kwa mwanaume ambaye hana mke, halafu urudi na mazawadi yale kama yote kweli?"

"Mmmh! Shoga yangu hizo sasa ni dhana. Na huo ni wivu. Wivu kwa Jerry na kwa mdogo wako. Mbona wewe umemkimbia, tena kwenye sherehe, leo wewe tena huyo, unaanza kumwoea wivu? Unamwonea wivu hata mdogo wako?"

**"Mmmh! Shoga yangu hizo sasa ni dhana. Na huo ni wivu. Wivu kwa Jerry na kwa mdogo wako. Mbona wewe umemkimbia, tena kwenye sherehe, leo wewe tena huyo, unaanza kumwoea wivu? Unamwonea wivu hata mdogo wako?"**

Vayajo alitulia kwanza. Akakaa kimya. Maneno yalionekana kumwingia. Kwa mbali kama vile alianza kujutia kitendo alichokifanya. Lakini akikumbuka milioni zake 10 ziko benki, akili ikamwambia kuwa alichokifanya ni sahihi. Anachotakiwa ni kupambana. Kupambana na mdogo wake Zulfa, halafu kumbembeleza Jerry.

"Naa utaniudhi. Mwenzako napambana kumrejesha Jerry kwenye mikono tangu, wewe ndiyo shoga yangu badala ya kunipa mawazo, wewe tena ndiyo unaninanga."

"Siyo kama nakunanga, kwanza hicho unachosema ni dhama, halafu hata kama ni kweli, wewe si uliondoka, na yeye hakutaka kwenda mbali. Na kama mdogo wako kakubali wewe utafanyaje? Na kwa hicho ulichomfanyia Jerry kweli atakubali tena uhusiano? Maana sijui sherehe zitafanyika tena, ndoa ifungwe, sijui itakuje, tutaanzia pale tulipoishia..." "Hizi kejeli sasa shoga yangu, kama huna cha kunisaidia nyamaza tu, unazidi kunitia hasira."

"Kwani umeshawahi kumpigia simu shemeji?"

"Ndiyo, lakini hapokei na wala nikituma meseji hajibu. Lakini Zulfa wanapigiana simu kila siku, mimi huwa nasikia wanavyoongea, wanaongea wenyewe wanacheka, inaniuma mimi." Vayajo akazidi kulalamika.

"Umeshawahi kukaa na mdogo wako unaongea naye kuhusu suala hilo?"

"Sijamwambia moja kwa moja hilo, lakini nilimpa 'advataizi' moja nilimfuata kisimani nikakutana naye njiani, nilimchamba, hukuwepo shoga malaika wako alikuwepo, sikumbakisha, halafu nikamsumia huko na ndoo yake ikamwagika. Ila mwenyewe hajui nini nimemfanyia hivyo, labda tu awe anahisi sababu ya kumfanya vile."

"Vibaya hivyo Vayajo, yule ni mdogo wako tu hata ufanye nini. Na haya yote ni kama wewe ndiye umesababisha. Ungekuwepo hata huyu Zulfa angeumwa na kuchukuliwa, angekaa kwako, haya yote yasingekuwepo, lakini kwa sababu amekaa kwa Jerry na kwa sababu yupo peke yake, unaona kama wamekuwa wapenzi. Mimi ushauri wangu mtafute mwenyewe Jerry, ukae naye uongee naye. Anaonekana kijana mstaarabu. Ndiyo maana hata ulipomtoroka, bado aliendelea kuwa na ushirikiano na familia yenu. Unajua ingekuwa mwingine angekata kabisa mawasiliano. Hata huku asingekuwa anakuja, achilia mbali kumtibia Zulfa. Kwanza wewe hukuwepo tu, huyo Zulfa ungemuona wakati ule anaumwa usingesema haya. Aliisha. Alikonda hata ukimtupia paka hamli. Kazi kafanya nani? Si huyu huyu shemeji? Shoga mtafute ongea naye. Sasa hapo tumia kila aina ya ushawishi kwa sababu akikataa tu hapo ujue imekula kwako. Kama atatafuta mwanamke mwingine dada, kama atakuwa ndiyo huyo huyo mdogo wako dada, mradi tu utakuwa umeula kwa chuya shoga."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# MARIOO HATAKI UFAHARI KUMWONA

SASA mwanamuziki anayetikisa Marioo ameonyesha kujali mashabiki wake baada ya kutangaza viingilio rahisi kuwahi kutokea katika matamasha yaliyoandaliwa na wasanii mbalimbali.

Marioo ambaye anatamba na kibao chake 'Bia Tamu' ametangaza kuwa shoo yake inayoitwa 'The Kid You Know' watu watafurahia kwa shilingi 300,000 pekee.

Tofauti watu wengi walivyotarajia pengine ingewabidi kutumia mamilioni ya pesa kupata tiketi, lakini mara ilipotangazwa baadhi walishindwa kuamini kama ni kweli.

# OMAR K AKAMILISHA 'UNDERGROUND FAME'

MSANII wa kizazi kipya, Omari K, amewataka wapenzi wa muziki huo kuichangamkia albamu yake mpya, Underground Fame, ambayo imetambulishwa jana.

Akizungumzia albamu hiyo, meneja wa Omari K, Mina Tz, amesema ndani ya Underground Fame, kuna ngoma 18 zilizoambatana na kolabo kadhaa.

Ndani ya albam hiyo wamo mastaa kama Khadija Kopa, Msami, Suma G, Ali Muya, Dyno Classic, Tee Lock, Dragon na Machine.

"Jana ulifanyika uzinduzi wa kuisikiliza albamu ya Underground Fame kule Louisville, Kentucky Marekani," amesema.

Tayari inapatikana kwenye mitandao yote ya muziki kama vile Dizzer, Spotify, BoomPlay, Amazon Music, YouTube, iTunes, Tidal na Google Play.



### CHELSEA, MOUNT WATETA
KLABU ya Chelsea imeongeza kasi ya jitihada za kuafikiana na kiungo wao, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24 kuhusu mkataba wake. Nyota huyo ananyemelewa na Liverpool. ***(Guardian)***

### FIRMINO KUBAKIA LIVERPOOL
LIVERPOOL iko katika mazungumzo na nyota wake, Roberto Firmino mwenye miaka 31 kuhusiana na kumpa mkataba wa muda mfupi. ***(Fabrizio Romano)***

### CAMAVINGA ANUKIA ARSENAL
ARSENAL inajipanga kumvuta kwa mkopo kiungo wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Eduardo Camavinga, ambaye ana umri wa miaka 20, awe sehemu ya kuimarisha kikosi chao ambacho kinaongoza katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England. ***(Evening Standard)***

### REUS KUTUA UNITED
MANCHESTER United inapiga hesabu za kumsajili kwa mkopo kiungo wa Borussia Dortmund, Marco Reus, ambaye ana umri wa miaka 33 baada ya Kocha Erik ten Hag kukutana na wakala wa mchezaji huyo. ***(Caught Offside)***

### TUCHEL AIKATAA SPURS
KOCHA wa Ujerumani, Thomas Tuchel hatazamii kuchukua usukani wa kuifunza Tottenham Hotspur endapo nafasi hiyo itajitokeza na badala yake ana mipango ya kujiunga na Barcelona au Real Madrid. ***(Florian Plettenber)***

### BELLINGHAM ASHAURIWA
KOCHA wa Borussia Dortmund, Edin Terzic, amemtaka, Jude Bellingham, ambaye ana umri wa miaka 19, "kuvunja minong'ono" na kukataa ofa za usajili kutoka Real Madrid na Liverpool. ***(Mirror)***

### LEICESTER YATUMA OFA
LEICESTER City imetuma ofa mpya kwa Stoke City ili kumnasa beki wake ambaye ni raia wa Australia, Harry Souttar, mwenye umri wa miaka 24, baada ya dau waliloliwasilisha awali la pauni milioni 10 kukataliwa. ***(Mail)***

### EMERY AMKATAA CHAMBERS
KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anatarajiwa kumwondoa katika kikosi chake beki, Calumn Chambers, ili aondoke katika harakati za kukifumua kikosi cha Villa - na hii itakuwa mara ya pili kwa kocha huyo kumwacha beki huyo mwenye miaka 28, mara ya kwanza alimwacha kwa sababu kama za sasa walipokuwa Arsenal. ***(Mirror)***

### FRANCA AWEKWA SOKONI
KLABU ya Newcastle United inaendelea na mazungumzo na Flamengo ili kuafikiana juu ya makubaliano ya kumsajili mshambuliaji kinda wa Brazil, Matheus Franca, ambaye ana umri wa miaka 18. ***(90min)***

### GUSTO ATAKIWA CHELSEA
KLABU ya Chelsea imeonyesha nia ya kumsajili beki wa kulia wa Lyon ya Ufaransa, Malo Gusto. ***(L'Equipe)***

### ZIYECH ATAJWA BARCA
Winga wa Timu ya Taifa ya Morocco, Hakim Ziyech (29), anatajwa huenda akajiunga na Chelsea au Barcelona katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa mwezi huu. ***(Sport - in Spanish)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED YAJIPANGA KUMSAJILI KANE

Bayern Munich, Madrid pia zatajwa kuingia katika vita hiyo ya kuwania...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuanza mchakato wa kumnunua nyota wa Tottenham Hotspur na nahodha wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwishoni mwa msimu huu.

Kane mwenye umri wa miaka 29, amekuwa na kiwango bora zaidi cha kufunga mabao akiwa na Spurs.

Amebakisha bao moja kumfikia Jimmy Greaves, kama mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo, huku tayari amemfikia Wayne Rooney kwa kufunga magoli mengi zaidi akiwa amevalia jezi ya England na anashika nafasi ya tatu kwa wafungaji wa mabao wa muda wote kwenye Ligi Kuu England.

Msimu huu umekuwa sawa, Kane ameanza mechi 20 za ligi katika kikosi cha Antonio Conte na kufunga mabao 15, akiwa nyuma ya Erling Haaland wa Manchester City mwenye magoli 22 katika mbio za kuwania kiatu cha dhahabu.

Tottenham hawana nia ya kuachana na mshambuliaji wao huyo ambaye anaweza kufikia uamuzi wa kwenda United, kwa sababu hali ya mkataba wake inaweza kulazimisha kuondoka.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Kocha wa United, Erik ten Hag, amemweka Kane juu ya mipango yake ya kumsajili mwishoni mwa msimu huu, wakati mchezaji huyo atakuwa na miezi 12 pekee katika mkataba wake.

Muhimu zaidi, ripoti hiyo inasema Kane yuko tayari kujiunga na Manchester United.

Spurs itadai ada ya angalau pauni milioni 85, huku gazeti la Bild likiongeza Bayern Munich na Real Madrid pia zinavutiwa na mshambuliaji huyo.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 1.89
X | 3.53
2 | 3.76

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ALVES ASHIKILIWA BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

MLINZI wa Brazil, Dani Alves, anashikiliwa kwa muda gerezani huku akisubiri uchunguzi kuhusiana na madai ya unyanyasaji wa kingono yanayomkabili, imefahamika.

Mlinzi huyo wa Barcelona, mwenye umri wa miaka 39, kwa mujibu wa BBC anadaiwa kumyanyasa mwanamke kwa kumgusa sehemu ya mwili wake kwa namna isiyofaa walipokuwa katika klabu ya usiku mjini Barcelona Desemba, mwaka jana.

Alves, ambaye alikana madai hayo, alipelekwa mahabusu na kuhojiwa na jaji mjini Barcelona, Ijumaa.

Klabu yake ya Mexico Pumas UNAM, ilikatisha mara moja mkataba wa Alves, kufuatia madai hayo.

"Klabu ilirejelea kusema haiwezi kuvumilia vitendo vya mmoja wao yoyote, hata awe nani, ambavyo vinakwenda kinyume na maadili ya klabu," alisema Rais wa Pumas, Leopoldo Silva.

"Hatuwezi kuruhusu mwenendo wa mtu mmoja kuharibu falsafa ya kazi yetu, ambayo imekuwa ya mfano wa kuigwa katika kipindi chote cha historia ya klabu."

Alves aliichezea Barcelona mechi 408 na pia alikuwa sehemu ya kikosi cha Brazil katika fainali zilizopita za Kombe la Dunia la 2022.

Polisi wa eneo hilo, Mossos d'Esquadra, amethibitisha taarifa ya kukamatwa na kufungwa kwa Alves kwa mashirika ya habari ya Reuters na AFP.

# Juventus yapokonywa pointi 15

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imepokonywa pointi 15 kutokana na uchunguzi wa awali kuhusu uhamisho wa klabu hiyo.

Shirikisho la Soka la Italia (FIGC) lilithibitisha habari hizo jana, huku Mkurugenzi wa zamani wa Juve, Fabio Paratici, ambaye sasa yuko Tottenham akifungiwa kwa muda wa miaka miwili na nusu kutojihusisha na soka la Italia.

Mwenyekiti wa zamani wa Juve, Andrea Agnelli, pia amepigwa marufuku kushikilia wadhifa wowote katika soka la Italia kwa miaka miwili ijayo.

Imeripotiwa uamuzi huo huenda ukakatiwa rufani na Juve.

Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Umma wa Turin ilikuwa ikitaka kukatwa pointi tisa kufuatia kusikilizwa kwa kesi mapema Ijumaa.

Lakini FIGC ilienda na adhabu kali zaidi baada ya Juve kugundulika walitumia uhamisho ili kuongeza mizania yao.

Adhabu hiyo inakuja nyuma ya mwenyekiti Agnelli, Makamu wa Rais, Pavel Nedved na wengine wa bodi ya Bianconeri kujiuzulu mwaka jana.

Hayo yalijiri baada ya uchunguzi kuanzishwa kuhusu ukiukaji wa fedha wakati wa uongozi wao.



CHEZA USHINDE KASINO

# BEKI MPYA ATUA YANGA, KUTAMBULISHWA KESHO

**Na Saada Akida**

HATIMAYE beki mpya wa kati wa Yanga, Mamodou Doumbia, amewasili nchini usiku wa kuamkia jana tayari kujiunga na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao kesho watavaana na Ruvu Shooting.

Yanga itamtambulisha Mamodou katika mchezo huo utakaopigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mamodou amekuja kuongeza nguvu katika safu ya ulinzi ya timu hiyo ambayo pia itashiriki mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Mwamba ameshafika na yuko kambini kuungana na wachezaji wenzake kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Ruvu Shooting, tutamtambulisha, kama ilivyokuwa kwa Kennedy Musonda," alisema Ally Kamwe, Ofisa Habari wa Yanga.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimekamilika na presha kubwa iliyobakia ni ya kupanga kikosi cha kwanza kutokana na ubora wa wachezaji aliokuwa nao.

"Presha kubwa sasa ni jinsi ya kutoa nafasi kwa kila mchezaji, hii inatokana na kikosi kukamilika vizuri, kila mchezaji anakuwa na afya njema, kuna kazi nzito ya kugawanya nafasi," alisema Nabi.

Kocha huyo amewataka wachezaji wake kuendelea kushindana kuanzia kwenye uwanja wa mazoezi kwa kujituma na kutumia akili ili kujihakikisha namba.

"Nawapongeza sana viongozi kwa kuunda timu kama hii ambayo kwanza ni gharama kubwa kupata watu bora kama hawa na kuwatunza, naona mambo mengi sio kitu rahisi," Nabi aliongeza.

Alisema kila mchezaji anatakiwa kujiandaa kutoa mchango wake katika mechi za mashindano yote zisizopungua 21 na kila mmoja anatakiwa kuongeza ushindani.



Bondia Karim Said 'Mandonga Mtu kazi' (kulia), akizungumza na wakazi wa Manispaa ya Morogoro waliojitokeza kumpokea katika eneo la kituo cha zamani cha daladala mkoani Morogoro. Hivi karibuni bondia huyo aliibuka mshindi katika pambano dhidi ya Mkenya, Daniel Wanyonyi lililofanyika Kenya. **PICHA: JOHN NDITI**

## Pambano la watani

INATOKA UK. 24

uliokuwa uchezwe Aprili 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya sasa utachezwa Aprili 9, mwaka huu, Namungo dhidi ya Mbeya City itachezwa Aprili 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, Lindi, Aprili 9, Dodoma Jiji wataikabili Coastal Union na KMC dhidi ya Geita Gold utachezwa Aprili 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Bodi hiyo iliahidi msimu huu hakutakuwa na mechi za viporo kwa ajili ya kupunguza lawama za upangaji wa matokeo au kulalamikia baadhi ya timu zinapendelewa.

## Nyota 9 nje Simba

INATOKA UK. 24

tika mechi iliyopita.

"Tunakwenda kucheza na moja kati ya timu bora sana Afrika, tutakutana na mechi ngumu, lakini sisi kama Dodoma Jiji tumejipanga kukabiliana na hilo. Mechi iliyopita na Geita Gold hatukufanya vizuri na nafasi tuliyonayo itatulazimu kufanya kila njia ili kuibuka na ushindi," alisema Liogope.

Baleke amesajiliwa Simba akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), lakini alikuwa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Nejmeh ya Lebanon wakati kiungo mkabaji, Ismael Sawadogo ametua nchini akitokea Difaa El Jadida ya Morocco na Mohamed Mussa amejiunga na Wekundu wa Msimbazi akitokea KMKM ya Zanzibar.

Wachezaji wa Simba watakaokosekana katika mechi ya leo ni pamoja na Sadio Kanoute, Mzamiru Yassin, Joash Onyango na Pape Sakho ambao wana kadi tatu za njano huku majeruhi wakiwa ni Moses Phiri, Peter Banda, Henock Inonga, Jonas Mkude na Chama.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba yenye pointi 47 ipo kwenye nafasi ya pili wakati Dodoma Jiji yenye pointi 21 ikiwa kwenye nafasi ya 12.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 22/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4025 | Port FC vs Bangkok Glass | 2.28 | 3.30 | 2.79 |
| 13:30 | 4632 | Gaziantep BB vs Sivasspor | 2.65 | 3.28 | 2.55 |
| 14:00 | 1132 | Chonburi vs BEC Tero Sasana | 1.65 | 3.69 | 4.47 |
| 14:15 | 1313 | Heerenveen vs Groningen | 1.73 | 3.61 | 4.45 |
| 14:30 | 2981 | Sampdoria vs Udinese | 3.42 | 3.18 | 2.11 |
| 15:00 | 3234 | Sunderland vs Middlesbrough | 2.78 | 3.23 | 2.43 |
| 15:30 | 1220 | Royal Antwerp vs Standard Liege | 1.71 | 3.68 | 4.57 |
| 16:00 | 1514 | Villarreal vs Girona | 1.71 | 3.86 | 4.41 |
| 16:00 | 1849 | Alanyaspor vs Fatih Karagumruk | 1.94 | 3.77 | 3.40 |
| 16:00 | 3233 | Kayserispor vs Besiktas | 3.22 | 3.54 | 2.07 |
| 16:30 | 1859 | Twente vs Utrecht | 1.72 | 3.78 | 4.28 |
| 16:30 | 5134 | Feyenoord vs Ajax | 2.63 | 3.37 | 2.48 |
| 16:30 | 5799 | Orlando Pirates vs Stellenbosch | 1.96 | 3.11 | 4.01 |
| 17:00 | 1255 | Manchester City vs Wolverhampton | 1.21 | 5.95 | 11.36 |
| 17:00 | 1943 | Ionikos Nikea FC vs AEK Athens | 10.60 | 5.51 | 1.25 |
| 17:00 | 2654 | Hibernian vs Hearts | 2.68 | 3.35 | 2.33 |
| 17:00 | 3389 | Leeds vs Brentford | 2.33 | 3.46 | 2.77 |
| 17:00 | 4431 | Hajduk Split vs HNK Sibenik | 1.22 | 5.14 | 11.31 |
| 17:00 | 5015 | Monza vs Sassuolo | 2.18 | 3.37 | 3.07 |
| 17:30 | 4724 | Borussia Dortmund vs Augsburg | 1.28 | 5.73 | 7.90 |
| 18:00 | 1350 | El Daklyeh vs Arab Contractors | 3.69 | 2.94 | 2.15 |
| 18:00 | 2037 | Al Hilal Riyadh vs Abha | 1.28 | 5.35 | 9.63 |
| 18:00 | 3002 | Levadiakos vs Lamia | 2.24 | 2.97 | 3.44 |
| 18:00 | 3032 | RFC Seraing vs Anderlecht | 5.18 | 3.93 | 1.59 |
| 18:00 | 5363 | Apoel Nicosia vs Akritas Chlorakas | 1.22 | 5.74 | 12.76 |
| 18:15 | 4557 | Elche vs Osasuna | 3.40 | 3.20 | 2.16 |
| 18:30 | 1171 | St. Gallen vs FC Basel | 2.29 | 3.65 | 2.75 |
| 18:30 | 3230 | Maritimo vs GD Estoril | 2.47 | 3.14 | 2.85 |
| 18:30 | 4949 | SuperSport Utd vs Richards Bay FC | 2.16 | 3.07 | 3.44 |
| 18:45 | 1032 | AZ Alkmaar vs Fortuna Sittard | 1.29 | 5.35 | 8.53 |
| 19:00 | 2035 | Adanaspor vs Yeni Malatyaspor | 1.87 | 3.47 | 3.63 |
| 19:00 | 4916 | AL Bataeh (UAE) vs Al Ain | 7.66 | 5.07 | 1.29 |
| 19:00 | 5535 | Trabzonspor vs Istanbulspor | 1.38 | 4.56 | 7.64 |
| 19:00 | 5896 | Dodoma FC vs Simba | 6.00 | 4.45 | 1.15 |
| 19:10 | 4856 | Vsnk Varazdin vs Lokomotiva Zagreb | 2.31 | 3.22 | 2.80 |
| 19:30 | 1398 | Monchengladbach vs Bayer Leverkusen | 2.62 | 3.71 | 2.33 |
| 19:30 | 3809 | Arsenal vs Manchester Utd | 1.89 | 3.53 | 3.76 |
| 20:00 | 1228 | Nea Salamis vs Omonia Nicosia | 3.99 | 3.57 | 1.85 |
| 20:00 | 5650 | Spezia vs Roma | 4.27 | 3.53 | 1.78 |
| 20:30 | 1232 | Panathinaikos vs PAOK | 2.17 | 3.01 | 3.54 |
| 20:30 | 1287 | Brugge vs Charleroi | 1.42 | 4.57 | 6.56 |
| 20:30 | 4603 | Barcelona vs Getafe | 1.21 | 5.82 | 14.13 |
| 20:30 | 4878 | Al Nasr Riyadh vs Al-Ettifaq | 1.27 | 5.35 | 10.27 |
| 21:00 | 1892 | Casa Pia Atletico vs Gil Vicente | 2.29 | 3.18 | 3.09 |
| 21:30 | 3270 | Atromitos vs Olympiakos | 7.01 | 4.46 | 1.41 |
| 21:45 | 1390 | Hermanstadt vs Steaua Bucuresti | 3.42 | 3.27 | 2.08 |
| 22:45 | 4506 | Juventus vs Atalanta | 2.17 | 3.23 | 3.23 |
| 23:00 | 1193 | Athletic Bilbao vs Real Madrid | 2.80 | 3.35 | 2.41 |
| 23:00 | 3077 | St Truiden vs KAA Gent | 3.29 | 3.34 | 2.12 |
| 23:30 | 1955 | Famalicao vs Rio Ave | 2.11 | 3.23 | 3.43 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Januari 22, 2023

Nipashe




**United yajipanga kumsajili Kane** UKURASA 21




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kulia), akipiga risasi juu kuashiria uzinduzi rasmi wa mashindano ya riadha ya wanawake 'First Ladies' yanayofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kudhaminiwa na Jaica. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nyota 9 nje Simba ikiivaa Dodoma Jiji

## ●●● Hata hivyo Robertinho aahidi burudani sasa itaanza kuonekana katika mechi...

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI Jean Baleke, Ismael Sawadogo na Mohamed Mussa waliosajiliwa na klabu ya Simba kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili wanatarajia kuonekana leo kwa mara ya kwanza kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma saa 1:00 usiku, timu hiyo itakapocheza mechi ya raundi ya 21 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwakosa wachezaji wake muhimu tisa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' alisema mechi ya leo itakuwa ni nafasi nzuri kwa timu yake kuelekea kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Robertinho alisema amejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu wapinzani wao pia wanahitaji ushindi ili kujiweka katika nafasi salama kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Nafikiri itakuwa nafasi nzuri kwa Simba kuelekea kwenye ubingwa wa Tanzania Bara, hii ni timu kubwa, tulikuwa na kambi nzuri Dubai na tukacheza vizuri, nilipata nafasi ya kuwajaribu wachezaji tofauti tofauti, tukarudi nchini tukacheza mechi yetu ya ligi, katika mechi ile (dhidi ya Mbeya City), kikubwa ilikuwa na kupata ushindi, kwa sababu tumeachwa pointi sita na wapinzani wetu wanaoongoza," alisema Robertinho.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili wachezaji hao wapya kama hawatakuwa na tatizo la kiafya, basi wataonekana dimbani kwa sababu wako tayari kwa mapambano na si vinginevyo.

"Dirisha dogo anasajiliwa mchezaji ambaye yupo tayari, haji kutayarishwa kwa hiyo ukiona mchezaji amesajiliwa kipindi kilichomalizika ujue moja kwa moja anakuja kutumika kama mlivyoona na Saido (Ntibazonkiza), nadhani hili limenyooka na linaeleweka, watacheza kwa uwezo wa Mungu kama hawataamka na matatizo, mtawaona uwanjani," alisema Mgunda.

Aliongeza watamkosa kiungo wao, Clatous Chama kwa sababu ni mgonjwa na si kutokana na jambo lingine lolote na ndio maana alitolewa mapema katika mchezo uliopita dhidi ya Mbeya City.

"Chama anaumwa, ni mgonjwa na hata alipocheza mechi yetu (dhidi ya Mbeya City) hakuwa mzima, alikuwa na malaria na mafua, tulimlazimisha, lakini baadaye tuliona ni kuendelea kumpa mzigo, ni lazima tuheshimu haki ya mtu kama binadamu, huwezi kuendelea kumchezesha mgonjwa ambaye unaona kabisa ameelemewa, " alisema Mgunda.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, alisema watafanya kila njia ili kupata pointi tatu wakiwa nyumbani kwa sababu wametoka kupata matokeo mabaya dhidi ya Geita Gold, ka-

INAENDELEA UK . 23

# Pambano la watani lapelekwa Aprili 16

**aada Akida na Adam Fungamwango**

MECHI ya watani wa jadi wa soka la nchini, Simba na Yanga iliyotarajiwa kuchezwa Aprili 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam sasa imesogezwa mbele hadi Aprili 16, mwaka huu, imefahamika.

Mabadiliko yako pia yamefanya baadhi ya mechi nyingine, zikiwamo za raundi ya 26 pia kubadilika.

Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, Karim Boimanda, aliliambia gazeti hili mchezo huo namba 184 umepangiwa siku nyingine kwa sababu wamepokea barua kutoka kwa wamiliki wa uwanja ikisema siku iliyopangwa awali kutakuwa na mkutano wa dini.

"Kwa maana hiyo pambano hilo la raundi ya 23, sasa litapigwa Aprili 16, mwaka huu kwenye uwanja huo huo kuanzia saa 11:00 jioni, Simba ikiwa mwenyeji," Boimanda alisema.

Alisema bodi pia imefanya mabadiliko katika mechi ya raundi ya 22 kati ya Geita Gold dhidi ya Coastal Union ambayo awali ilikuwa ichezwe kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Februari 4, mwaka huu, imerudishwa nyuma hadi Januari 24, mwaka huu.

Aliongeza mechi za raundi ya 26 ambazo kwa mujibu wa bodi nazo zimebadilishiwa tarehe baada ya mabadiliko ya mechi ya 'dabi' ni kati ya Singida Big Stars dhidi ya Polisi Tanzania ambayo itacheza kwenye Uwanja wa Liti, Singida ifikapo Aprili 7, mwaka huu wakati pambano kati ya Yanga dhidi ya Kagera Sugar ambalo lilikuwa lichezwe kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Aprili 16, mwaka huu sasa litapigwa hapo hapo, lakini ni Aprili 7.

Ihefu watawakaribisha Simba kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya sasa itachezwa Aprili 8 wakati Azam dhidi ya Mtibwa kwenye Uwanja wa Azam Complex itafanyika ifikapo Aprili 8, mwaka huu.

Mechi nyingine za raundi hiyo zilizoathirika na ratiba hiyo ni Prisons dhidi ya Ruvu Shooting

INAENDELEA UK . 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >